SUPA JACKPOT
TZS. 1,142,132,257
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Abambwa** gesti akiwa na vipande meno ya tembo

UKURASA 3




UKURASA 9


Nipashe JUMAPILI
MWANGA WA JAMII
Jumapili Agosti 13, 2023 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • No. 0581401
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# KUMEKUCHA

## MWABUKUSI,

Mdude mbaroni tuhuma za uchochezi, ni baada ya IGP...

*Endelea ukurasa. 2*



Mdude Nyagali Mpaluka

Wakili Boniface Mwabukusi



Eneo la Mwenge, Dar es Salaam lililokuwa maarufu kwa pilikapilika za wafanyabiashara wadogo, maarufu kama Machinga, likiwa wazi jana jioni tofauti na awali baada ya mgambo wa Manispaa ya Kinondoni kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi, kuwaondoa wasaka riziki hao. **PICHA: JOHN BADI**

UKURASA WA 4

## MWAPACHU AZINDUA KITABU SAFARI YA MITO, MILIMA,MABONDE MAISHA YAKE

MWANADIPLOMASIA Balozi Juma Mwapachu, amezindua kitabu chake 'A Journey (My life, Speeches and Writings) ambacho kimeeleza...

## Waziri Mkuu ageuka mbogo ucheleweshaji mafao wastaafu

UKURASA 2

# Mkanganyiko matibabu bure malaria

UKURASA 3

MICHEZO SIMBA, YANGA HESABU MEZANI UK.24
MAONI, KATUNI UK.6

## HABARI KITAIFA



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akiwa na mkewe Mama Mariam Mwinyi (kulia kwake), wakimsikiliza kijana Idrisa Haroub Addi wa kikundi cha vijana cha Classic Design kutoka Chukwani Unguja, akitoa maelezo ya michoro ya majengo ya bustani ya Forodhani na jengo la Marikiti Kuu Darajani, alipotembelea maonyesho wakati wa maadhimisho ya kilele cha Siku ya Vijana Kimataifa katika viwanja vya Maisara Suleiman, Wilaya ya Mjini Unguja, jijini Zanzibar jana. Kushoto kwake ni Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Zanzibar, Tabia Mwita. **PICHA: IKULU**

# Mwabukusi, Mdude mbaroni tuhuma uchochezi

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini linawashikilia Wakili Boniface Mwabukusi na Mpaluka Nyagali, maarufu kama Mdude, kwa mahojiano.

Mwabukusi na Mdude wanahojiwa kwa tuhuma ambazo awali walizieleza ni za kuandaa na kutoa maneno ya uchochezi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Jeshi hilo, Kamishna msaidizi mwandamizi (SACP) David Misime, polisi waliwakamata watuhumiwa hao maeneo ya Mikumi, mkoani Morogoro usiku wa kuamkia jana, majira ya saa 8:30 usiku.

"Jeshi la Polisi kama lilivyoeleza jana (juzi), linafuatilia ili liwakamate watuhumiwa walioandaa na kutoa maneno ya uchochezi, kazi hiyo inaendelea kufanyika kwa mujibu wa sheria.

"Hadi sasa, jeshi limefanikiwa kuwakamata Boniface Anyasile Mwabukusi na Mpakula Nyagali, maarufu kama Mdude, na mahojiano yao yanaendelea," alisema Misime.

Juzi, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, aliitisha mkutano na waandishi wa Habari Dar es Salaam na kutoa onyo kali kwa watu au kikundi kinachopanga kufanya maandamano nchi nzima ili kuiangusha serikali kabla ya uchaguzi mkuu mwaka 2025.

Wambura alisema watu wanaotaka kufanya hivyo, kamwe wasiingie katika mtego huo kwa kuwa watashughulikiwa na dola ipasavyo.

IGP Wambura alisema wakati wanatoa taarifa hizo za ajabu, watu hao wanahusisha maandamano na kushawishi jumuiya ya Watanzania kuwaunga mkono na hoja zinazoendelea za bandari.

"Tuliamini hoja za bandari hujibiwa kwa hoja na vile vile tuliamini kwa sababu baadhi ya watu hawa walikwenda mahakamani basi wangeheshimu uamuzi wa mahakama. Badala yake, wametoka na kuanza kutafuta ushawishi na kuchochea kuwataka Watanzania waingie kwenye maandamano ya nchi nzima.

"Lakini mmoja amekwenda mbali zaidi akieleza watahakikisha wanaiangusha serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kabla ya mwaka 2025. Huu ni uhaini. Jambo la kwanza tunawahakikishia watu hawa wakome kabisa na wasitishe matamshi yao," alionya IGP Wambura. Alisema watakaofanya hivyo watachukuliwa hatua za kisheria kwa uchochezi wanaoufanya na uhaini walioupanga yote ni makosa ya jinai.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
13.08.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumatano tarehe 16-08-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Kilombero,** gari hilo lina namba za usajili: **T 835DSC/T879EAU**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita 20.40** |
| **Upana** | - | **mita 4.20** |
| **Kimo** | - | **mita 5.40** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Chalinze hadi Kilombero** kupitia **Mikumi,** gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**


# Waziri Mkuu ageuka mbogo kwa ucheleweshaji mafao watumishi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameelezea kukerwa na ucheleweshaji wa mafao ya watumishi unaofanywa na mifuko ya hifadhi ya jamii, huku akiwakumbusha watumishi wa taasisi hizo watambue kuwa ni wastaafu watarajiwa.

Aidha, ili kuhakikisha kero hiyo inabaki historia, ametoa maagizo 10 ikiwamo mifuko yote ya hifadhi ya jamii kulipa mafao kwa wakati na kwa mujibu wa sheria ili kuleta utulivu kwa wanachama na wastaafu.

Pia ameagiza wazee wastaafu kutosumbuliwa na watumishi wa mifuko ya hifadhi ya jamii, hivyo waendelee kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa umma.

Majaliwa alisema hayo jana wakati wa maadhimisho ya miaka mitano ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na uzinduzi wa huduma za wanachama kidijitali, jijini hapa.

"Wazee wastaafu wasisumbuliwe. Kumbukeni kuwa sisi sote ni wastaafu watarajiwa," alisema Majaliwa.

Maagizo mengine aliyotoa kwa mifuko hiyo ni kuhakikisha inafanya uwekezaji wenye tija kwa wanachama na jamii inayolingana na thamani ya fedha za wanachama.

"Fanyeni utafiti wa kina kubaini masoko ili uwekezaji unaofanywa usilete hasara kwa mifuko," aliagiza.

Pia aliutaka mfuko wa PSSSF uendelee kutoa elimu kwa wanachama na umma ili kujenga uelewa sahihi na hivyo kupunguza malalamiko.

Alisema mfuko huo unatakiwa kuweka utaratibu maalum wa kuwafikia na ikiwezekana katika zile taasisi ambazo wana wanachama wengi.

"Katika hotuba yangu ya kuhitimisha Bunge la Bajeti Juni 28, 2023 nilielekeza waajiri wote watunze kumbukumbu za malipo ya michango ya waajiriwa pamoja na kulipa malimbikizo ya michango ya watumishi na tozo katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ifikapo Septemba 30, mwaka huu. Na leo ninarudia kusisitiza agizo langu, tarehe 30 Septemba madai yote yanayohusu upande wa waajiri yawe yamekamilishwa," alisisitiza.

Kadhalika amewataka waajiri wote wahakikishe wanalipa michango ya wanachama kwa wakati ili kuondokana na usumbufu wakati wa kulipwa mafao.

Alisema mafao ya wastaafu ni haki yao ya msingi hivyo, waajiri wasiwe kikwazo kwa Mifuko ya Hifadhi ya jamii kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa utaratibu waliojiwekea.

"Watendaji wa PSSSF ongezeni ufanisi zaidi ili mwendelee kuwa taasisi ya mfano kwa kuvutia taasisi mbalimbali ndani na nje ya nchi kuja kujifunza na kubadilishana uzoefu," alisema.

Vilevile, aliwataka watendaji wote wa PSSSF, kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu ili kulinda mafanikio yaliyopatikana na kuendeleza rekodi zaidi ya mafanikio.

"Watanzania waliojiajiri wenyewe jiwekeeni akiba ili msiachwe kando na kukosa fursa ya kuwa na maisha ya staha ambayo ni stahili ya kila binadamu," alisema.

Alimwagiza Mwenyekiti wa Bodi ya PSSSF, Menejimenti na Watumishi wote wa mfuko huo kuendeleza jitihada na ubunifu zaidi wa kidijitali ili kufikia malengo waliyojiwekea.

"Ili kukomesha vitendo vya utapeli wa mafao ya wastaafu unaofanywa na watu wasio na mapenzi mema, mfuko uanzishe namba maalum na kuitangaza kwa umma ili kuondoa usumbufu kwa wastaafu kwa kuwa wapo matapeli wanaopiga simu za ulaghai wakidai wao ni wafanyakazi wa PSSSF," alisema.

Hata hivyo, aliwataka wanachama wa mifuko walioko kazini, waweke utaratibu wa kutembelea Ofisi za mifuko yao ili kuona kama taarifa zao ziko sawa.

"Katika hili mifuko ya hifadhi iweke utaratibu mwepesi wa kupata taarifa, pia kupitia kwa kutumia teknolojia zilizopo," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa maono na dhamira ya dhati ya kuimarisha sekta ya hifadhi ya jamii.

"Lengo la Rais Samia ni kuona inafanya kazi kwa tija, ufanisi na kutoa huduma bora, tunampongeza pia kwa mfumo wa hati fungani wa Sh. trilioni 2.17 za kulipa deni ambalo limedumu kwa muda mrefu, mfumo huu umewezesha PSSSF kulipa wastaafu kwa wakati," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, CPA Hosea Kashimba, alisema kwa kipindi cha miaka mitano, hadi kufikia Juni, mwaka huu, mfuko huo umelipa kiasi cha Sh. trilioni 8.88 kwa wanufaika 262,095.

Alisema kati ya Julai, 2018 na Juni, mwaka huu, mfuko huo umelinda na kuongeza thamani yake kwa asilimia 27.76 kutoka Sh. trilioni 5.83 hadi Sh. trilioni 8.07 Juni, 2023.

"Ongezeko hili ni sawa na wastani wa asilimia 6.72 kwa kila mwaka," alisema Kashimba.



Mkuu wa mkoa wa Arusha, John Mongela (kulia), akizungumza na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi wa kwanza, Jenerali mstaafu Mirisho Sarakikya, alipomtembelea ili kumjulia hali nyumbani kwake, Meru wilayani Arumeru jana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mkanganyiko matibabu bure malaria

**Na Waandishi Wetu**

AGIZO la serikali kutaka huduma za vipimo, dawa na sindano kwa wagonjwa wa malaria zitolewe bure, limeibua mkanganyiko katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Mkanganyinko huo unatokana na baadhi ya maeneo agizo hilo kutekelezwa kama lilivyotolewa huku baadhi ya maeneo watoa huduma wakikiri kwamba hawajaanza kutekeleza kutokana na kutopata utaratibu mwingine na wengine kupanga kuanza mwezi ujao.

Hatua hiyo imesababisha wananchi katika baadhi ya mikoa kulalamikia kutozwa fedha kwa huduma hiyo. Wiki iliyopita, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, aliwataka wataalam waache kitu alichokiita 'uhuni' kuhusu suala la tiba ya malaria huku akiwataka wananchi wanaolipishwa huduma hizo kutoa taarifa katika mamlaka husika ili hatua zichukuliwe.

Akizungumza na Nipashe, mkazi wa Kijiji cha Kigwe, Bahi mkoani Dodoma, Meshack Masinga, alisema kauli iliyotolewa na Waziri Ummy ni jambo jema kwao lakini bado katika maeneo yao haijaanza kutekelezwa.

"Huku kwetu (Bahi) bado huduma za malaria tunalipia vipimo, dawa na sindano lakini kama watasimamia na agizo lilivyosema, itakuwa jambo jema kwa wagonjwa malaria kupata huduma bure ili kufikia azma ya kumaliza ugonjwa huu nchini," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Hopitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Dk. Ernest Ibenzi, alisema wamekuwa wakitekeleza utaratibu huo wa kutoa huduma hiyo bure.

"Alichokisema Waziri Ummy tumekuwa tukikitekeleza katika hospitali yetu. Tunatoa vipimo, dawa na sindano bure kwa wagonjwa wa malaria. Wagonjwa wanaandikiwa na kupata matibabu bure," alisema.

Dk. Ibenzi alisisitiza kuwa dawa ambayo hutolewa bure hivi sasa ambayo inatibu ugonjwa wa malaria ni ARU na kwamba wako katika mchakato wa kuongeza zingine ambazo zitakuwa zinatolewa bila malipo kwa wagonjwa.

"Tuko katika mchakato wa kuongeza dawa zingine zile za juu ili kuendeleza jitihada za serikali kukomesha Malaria katika maeneo yetu," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Catherine Magali, alisema bado hawajaanza kutekeleza matibabu na vipimo bure vya malaria na kwamba huduma hiyo wanatarajia kuianza mwezi ujao baada ya kuweka utaratibu.

Mtaalamu wa afya mkoani Kilimanjaro (jina tunalo), alisema bado hawajapewa mwongozo wowote utakaosaidia utekelezaji wa jambo hilo.

"Yule (Waziri) kwetu ni kiongozi, ametoa maelekezo lazima kutakuwa na mpango bora wa utekelezaji ingawa kwa sasa bado haujatufikia, ila endapo utatufikia tutautekeleza kwa sababu hapa kuna ununuzi wa vifaa vitakavyotumika kufanya hivyo," alisema.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Dk. Paschal Mbota, alisema wilayani humo tayari wameanza kutoa huduma bure ya vipimo vya malaria kupitia kipimo cha MRDT.

Ernest Emmanuel, mkazi wa Manispaa ya Moshi, alisema utekelezaji wa agizo hilo unaleta unafuu wa maisha kwa wananchi kutokana na matibabu kuwa na gharama kubwa.

"Kilichotangazwa ni furaha kwa wananchi lakini ni uchonganishi kwa kuwa tunaamini serikali haijatoa mwongozo wowote wala rasilimali fedha, hivyo mtu anapofika hospitalini atataka huduma hiyo. Huu ni uchonganishi," alisema.

Mgonjwa aliyekuwa akipatiwa matibabu katika Kituo cha Afya cha Pasua, Manispaa ya Moshi, Mwanaisha Hassan, alisema bado agizo hilo halijaanza kutekelezeka.

"Leo nilikuwa ninapatiwa matibabu hapa Pasua, nimeulizia kama ninaweza kupata huduma ya kipimo cha malaria bure baada ya kuona serikali imesema hivyo, nikajibiwa hawajapewa mwongozo huo," alisema.

Katika Mkoa wa Tanga, Mganga Mkuu wa Mkoa huo, Dk. Japhet Simeo, alisema wao wanatoa huduma hiyo bure pamoja na dawa.

Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Mji wa Babati, Dk. Peter Kyabaroti, alisema wanatekeleza agizo hilo kwa muda mrefu sasa linalolenga kuunga jitihada za kutokomeza ugonjwa wa malaria.

Katibu wa Afya wa Hospitali ya Rufani ya Mwananyamala, Dar es Salaam, Rajabu Kaseke, alisema wanatekeleza agizo hilo kwa vitendo kwa upande wa vipimo na utoaji wa dawa.

## Abambwa na meno ya tembo gesti

**Na Friday Simbaya,**
IRINGA

JESHI la Polisi mkoani Iringa limewakamata watu wawili kwa matukio mawili tofauti likiwamo la kukamatwa na vipande saba vya meno ya tembo.

Watu hao wamekamatwa wakati polisi wakifanya doria na misako mbalimbali ili kubaini, kuzuia na kupambana na uhalifu.

Katika tukio la kwanza, Jacob Mhanga (54) mkazi wa kijiji cha Utiga mkoani Njombe, amekamatwa akiwa na vipande saba vya meno ya tembo katika nyumba ya kulala wageni katika Kijiji cha Mbalamaziwa, Mufindi mkoani Iringa.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Iringa, Kamishna Msaidizi (ACP) Allan Bukumbi, alisema juzi kuwa mtuhumiwa alikamatwa Agosti 8, mwaka huu, akiwa na vipande saba vya meno ya tembo.

Tukio la pili, alisema jeshi hilo kwa kushirikiana na askari wa uhifadhi, kupitia taarifa fiche kutoka kwa raia wema, lilimkamata Mathias Malenga (37) mkazi wa Image, wilayani Kilolo akiwa na silaha mbili ndani ya nyumba yake, moja shotgun na gobore.

Alisema tukio hilo lilitokea Agosti 6, mwaka huu, majira ya saa 1:00 usiku, mtuhumiwa huyo alikamatwa na shotgun ikiwa na risasi mbili na maganda matatu na gobore likiwa na goroli sita na mtego wa kuwindia wanyama.

Kamanda Bukumbi alisema watuhumiwa wote watafikishwa mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

Katika hatua nyingine, watuhumiwa 11 wamefikishwa mahakamani na kuhukumiwa kwa makosa mbalimbali. Washtakiwa hao ni Naftar Lyandala (40) mkazi wa Uhambingeto ambaye Juni 27, mwaka huu amehukumiwa kifungo cha kunyongwa hadi kufa kwa kosa la mauaji, Francis Masoud (41) mkazi wa Kitasengwa, Denis Mtega (31) mkazi wa Ilula Mtua na Emmanuel Nzogela (29) mkazi wa Ipogolo kwa nyakati tofauti wamehukumiwa kifungo cha miaka 30 jela kwa makosa ya kubaka.

Watuhumiwa wengine, Godfrey Chengula (33) mkazi wa Isakalilo amehukumiwa kifungo cha mwaka mmoja jela kwa kosa la kutoroka chini ya ulinzi na Batros Kipako (47) amehukumiwa mwaka mmoja jela kwa kosa la kupatikana na silaha (gobore).

Aidha, Musa Mtung'e (35) mkazi wa Idodi amehukumiwa kifungo cha miaka mitano jela kwa kosa la kujaribu kubaka, Prudence Patrick (24) mkazi wa TRM Kihesa amehukumiwa kifungo cha miaka saba kwa kosa la mauaji na Desderia Mbwelwa (52) mkazi wa Lumuli, Ifunda amehukumiwa kifungo cha miaka 26 kwa kosa la shambulio la aibu dhidi ya mtoto.

Emmanuel Mahundi (31) mkazi wa Ibumu wilayani Kilolo amehukumiwa kifungo cha maisha jela kwa kosa la kubaka pamoja na fidia ya Sh. 500,000 na God Kunzungula (41) mkazi wa Ipilimo, Mufindi amehukumiwa miaka 30 jela kwa kosa la unyang'anyi wa kutumia silaha.


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA YA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO
WILAYA YA MOROGORO
KITUO CHA MJINI, MKOA WA MOROGORO

Usimamizi wa Mirathi Na......83/2023

KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: ELIZABETH PAUL CHAYA WA KIHONDA AIRPORT

KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: AZARIA TANDA CHANYA

**TANGAZO**

(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 21 Mwezi 08 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;
- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehem anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

**Imetolewa leo tarehe 07 mwezi 08 mwaka 2023**

HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**DESMOND DESDERY BIKOME** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **NISSAN PRIMERA** usajili namba: **T107 DKT,** CHASSIS NAMBA: **QP12007843** na ENGINE NAMBA: **QG18260151A.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/270270/2023**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**DR LOUIS BERNARD MLINGI** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 608 BPB** (CHASSIS NO **AT2116056134)** CARINA jina la kwenye kadi ya Gari ni **LASTING LAST CALL LTD** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi **MOR/MOR/RB/171969/2023.**

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**DR LOUIS BERNARD MLINGI** Anatangaza kupotelewa na kadi ya Gari yenye namba za usajili **T 177 BNA** (CHASSIS NO **NZE1203028382) TOYOTA CORROLA** jina la kwenye kadi ya Gari ni **LASTING LAST CALL LTD** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi **MOR/MOR/RB/171985/2023.**

## Biteko: Rais Samia kielelezo maendeleo

**Na Mwandishi Wetu,** BUKOMBE

RAIS Samia Suluhu Hassan ametajwa kuwa kiongozi mahiri katika kipindi cha muda mfupi huku akionyesha mageuzi makubwa ya maendeleo.

Katika kipindi cha muda mfupi alichokaa madarakani, imeelezwa kuwa kazi aliyoifanya haina mfano, hivyo Watanzania wanatakiwa kuendelea kumwamini na kumpa muda kwa kuwa kuna mambo makubwa ya maendeleo anaendelea kuyafanya.

Waziri wa Madini, Dk. Doto Biteko, alisema hayo jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika Runzewe katika wilaya ya Bukombe ikiwa ni mwendelezo wa mikutano iliyoandaliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Geita kuelezea utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya chama hicho kwa mwaka 2020-2025.

Biteko ambaye ni Mbunge wa Bukombe na Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM, alisema katika muda mfupi aliokaa Rais Samia madarakani, mambo mengi yamefanyika hususan katika miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa barabara, miundombinu ya elimu, afya na maji. "Huduma zote kwa wananchi zimeimarika, hivyo Rais Samia anatakiwa kupimwa kwa kipimo cha mapenzi mema kwa Watanzania, kwenye uendelezaji wa miradi ya maendeleo, kwa kuleta utulivu katika nchi, pamoja na kuimarisha demokrasia nchini.

"Rais Samia amewafanya Watanzania kila mmoja kujiona daraja la kwanza kwenye nyanja zote za kilimo, biashara, madini na kadhalika. Mama huyu amepiga kazi kubwa sana," alisema Biteko.

Dk. Biteko alisema tangu amechaguliwa kuwa mbunge ataendelea kuwa wakili mwaminifu kutoa ushuhuda kwa wananchi kwa mambo yaliyofanywa na serikali katika jimbo la Bukombe.

Alisema jimbo la Bukombe kabla ya CCM kushika hatamu liliwahi kuongozwa na upinzani na ilikuwa wilaya ya mwisho kwenye kila eneo kwenye sekta mbalimbali za maendeleo katika mkoa wa Geita.

"Kwa sasa wilaya inapaswa kupimwa kwa namba. Unaweza ukamchukia Rais Samia lakini namba zikamtetea. Wilaya yetu tumetoka kwenye zahanati tatu sasa kuna zahanati 11, maboma mapya ya zahanati mpaka sasa 22 yanajengwa, kutoka vituo vya afya viwili mpaka saba, kupandisha hadhi kituo cha Afya cha Uyovu kuwa hospitali"

"Tumerithi hospitali ya Wilaya ikiwa na hadhi kama zahanati, tumeipandisha kwa kujenga majengo mapya, majengo ya dharura, jengo la mama na mtoto. Tumetoka kuwa na shule moja ya kidato cha tano na sita mpaka kuwa nazo tano," alisisitiza.

# Mwapachu azindua kitabu safari ya mito, milima,mabonde maisha yake

**Na Beatrice Shayo**

MWANADIPLOMASIA Balozi Juma Mwapachu, amezindua kitabu chake 'A Journey (My life, Speeches and Writings) ambacho kimeeleza maisha yake tangu utotoni na mchango alioutoa katika maendeleo ya taifa.

Akizindua jana jijini Dar es Salaam kitabu hicho, aliyekuwa Balozi wa Tanzania nchini Afrika Kusini, Ami Mpungwe, alisema utamaduni wa baadhi ya watu waliochangia maendeleo ya taifa yasipowekwa kimaandishi yatapotea na itakuwa hasara kubwa kwa vizazi vijavyo.

Kitabu hicho kina kurasa 600 na kwa nakala ngumu kinauzwa Sh. 100,000 na nakala laini Sh. 70,000.

"Kwa mafano sisi wengine tulikuwa kwenye nyanja za diplomasia huko wakati ule wa ukombozi. Mambo mengi ya historia watayatafuta bila kutambua kama wale waliohusika au tuliohusika hatuandiki, tutajikuta tunaondoka nayo kwenda kaburini," alisema Balozi Mpungwe.

Alisema tukio hilo ni muhimu kwa sababu linadhihirisha umuhimu wa kujenga jamii ya Tanzania kuwa na utamaduni wa kuandika na kuweka kwenye kumbukumbu michango yao tofauti katika maendeleo ya taifa.

Alisema kwa Balozi Mwapachu si mara yake ya kwanza kuandika kitabu kwa kuwa amekuwa mwandishi nguli katika fani hiyo.

Mpungwe alisema kitabu hicho kilichozinduliwa kina umuhimu wa pekee kwa kuwa kimelenga kuelezea maisha yake tangu alipokuwa mdogo, elimu, kazi na nyadhifa mbalimbali alizoshika.

"Wengi hawamfahamu Balozi Mwapachu. Alianza kazi kama askari polisi. Hakudumu kwa muda mrefu na baadaye alikwenda kufanya kazi Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa muda mfupi na kwenda kufanya kazi baada ya kuanzishwa sera ya madaraka mkoani," alisema.

Balozi Mpungwe alisema Balozi Mwapachu amefanya kazi serikali, ubalozini, sekta binafsi na amekuwa mchangiaji mzuri wa maendeleo ya nchi. "Kitabu hiki kina umuhimu kimekusanya kwa pamoja uzoefu na maisha ya Balozi Mwapachu, michango yake katika maendeleo ya taifa letu. Yote yamo katika kitabu kimoja, uzoefu wake na safari yake na makala mbalimbali alizoziandika," alisema.

Alisema tukio hilo linatoa chachu na mwito kwa watu kujenga utamaduni wa kuandika kwa faida ya vizazi vilivyopo na vijavyo.

Mwanasheria nguli, Prof. Issa Shivji, alitoa pongezi kwa Balozi Mwapachu kwa kitendo cha kuendelea kuandika vitabu na kuachia urithi wa tafakuri yake kimaandishi.

Hata hivyo, alisema mitandao ya kijamii haiwezi ikawa mbadala wa vitabu kwa kuwa kuna raha ya (mtu) kushika kitabu na kusoma.

"Rafiki yangu Juma hakuingia kwenye mitego kwa kushawishika kuingia kwenye siasa ndiyo maana amebaki kuwa mwanazuoni. Kwa maoni yangu, ukiingia kwenye siasa na kuwa mwanasiasa wengi wanaacha kuwa wanazuoni," alisema Shivji.

Prof. Shivji alisema katika maisha yake alikuwa na nafasi nyingi za kuingia katika siasa lakini alikataa na ameendelea kuandika na kufanya mambo mengine ikiwamo kuanzisha jarida la Change. Kwa upande wake, Balozi Mwapachu alisema kilichosababisha kuandika kitabu hicho ni historia ya urithi wa baba yake ambaye alikuwa rafiki mkubwa wa Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere.

"Nilikaa na kutafakari ni kwa namna gani nitaandika kuhusu maisha yangu. Nikaona niandike kuhusu kuzaliwa, kazi nilizozifanya na mchango wangu wa maendeleo na zipo makala nilizokuwa naziandika nimezielezea katika hiki kitabu," alisema.

Balozi Mwapachu amehamasisha vijana na wale walio na umri kama wake waandike vitabu kuhusu masuala ambayo wanayaona ni muhimu katika nchi.

"Mfano 1986 niliandika kitabu kilichochapishwa nchini India. Nilitazama maendeleo ya mashirika ya umma hapa nchini, changamoto wanazozipata kulikuwa kuna kudhani kuwa shirika ambalo lipo na serikali haliwezi kuanguka.

"Kumbe serikali ilikuwa inaliingilia kwa undani na kuyafanya mashirika yafe si kwa nia mbaya, isipokuwa ni kwa kubadilisha sera kila wakati au kutaka kuwaingilia waendeshaji," alisema Balozi Mwapachu na kuwaomba Watanzania kununua kitabu hicho na kujifunza mambo mbalimbali.



Msamaria mwema asiyejulikana akiwa ameweka tawi la mti kwenye shimo lililo wazi barabarani katika Mtaa wa Samora, jijini Dar es Salaam jana, ili kuwapa tahadhari waendesha vyombo vya moto. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Upinzani waonywa siasa za chokochoko

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Umoja wa Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (UVCCM) Taifa, Mohamed Ali Kawaida, ameviyonya baadhi ya vyama vya upinzani kutokana na kuendesha siasa za chokochoko zinazolenga kukwamisha juhudi za maendeleo.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika uwanja wa Chaani, Mkoa wa Kaskazini Unguja jana, alisema UVCCM itaendelea kulinda, kutetea na kusimamia maslahi ya serikali zinazotokana na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Kawaida alivikumbusha vyama hivyo vya upinzani kuwa kizazi kilichofanya mapinduzi ya Zanzibar mwaka 1964 bado kipo hai na sasa kimejielekeza katika utetezi wa chama, serikali na viongozi wake.

"Nasaha zangu kwa upinzani, wasitumie vibaya fursa ya mikutano ya hadhara kama kichaka cha kutekeleza mipango yao miovu dhidi ya serikali, badala yake watoe ushauri na maoni ya kuibua hoja na changamoto zinazowakabili wananchi ili zitafutiwe ufumbuzi" alisema Kawaida.

Alisema serikali inaendelea kufanya mambo mengi ya maendeleo kwa nia ya kumaliza changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi wa mijini na vijijini.

Kawaida alifafanua kuwa makubalino ya uwekezaji baina ya kampuni ya DP World na Bandari ya Dar es Saalam yana maslahi makubwa ya kuimarisha uchumi wa nchi.

Alisema utatuzi wa kero na changamoto za wananchi mijini na vijijini ndiyo kielelezo cha ushindi wa CCM katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Kaimu Katibu Mkuu wa UVCCM, Mussa Haji Mussa, aliwasihi wananchi kupuuza upotoshaji unaofanywa na Chama cha ACT Wazalendo wanaodai mkoa huo umetelekezwa na hauna maendeleo.

Wajumbe wa Kamati ya Utekelezaji ya UVCCM Taifa, wakiwamo wabunge, wawakilishi na wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM kutoka katika umoja huo walisema serikali zote mbili ya Muungano na Zanzibar zimetekeleza kwa ufanisi Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 - 2025.

HABARI KITAIFA

# Waokolewa baada ya kufukiwa na kifusi mgodini kwa siku 10

**Na Renatus Masuguliko,** GEITA

WACHIMBAJI wawili waliofukiwa na kifusi kwa siku 10 katika mgodi wa dhahabu wa Igalula, Nyang'hwale mkoani hapa, wameokolewa wakiwa hai.

Mchakato wa kuwanasua kutoka katika kifusi ulifanyika Alhamisi na kwa kipindi chote wameeleza walikuwa wakinywa mkojo wao.

Akisimulia tukio hilo, Mkurugenzi wa Mgodi huo, Hussein Makubi, alisema tukio la kufukiwa na kifusi lilitokea Agosti Mosi, mwaka huu, baada ya watu watatu kuingia kwa njia za panya katika shimo hilo lenye urefu wa zaidi ya mita 200 lililokuwa limezuiwa.

Makubi alisema mmoja kati yao, alifanikiwa kutoka baada ya kuwaacha wenzake ambao ndio wameokolewa wakiwa hai na sasa wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Wilaya ya Nyang'hwale kutokana na miili yao kudhoofika.

Alisema baada ya kufanikiwa kutoka ndipo alipotoa taarifa mgodini na juhudi za kuwanasua waliokwama kwenye kifusi zilipoanza. Manusura wa ajali hiyo, wakizungumza na mwandishi wa habari hii hospitalini, walisema baada ya kukaa muda mrefu ndani ya shimo hilo waliingiwa na hofu ya kifo na kulazimika kuanza kunywa mkojo na kula udongo kukabiliana na njaa.

Mpina Shukuru (19), mkazi wa wilaya ya Chato mkoani Geita, alisema baada ya kukaa humo muda mrefu, walikata tamaa na hawakujua kama wangepata msaada.

Renatus Nyanga (35), mkazi wa Sengerema mkoani Mwanza, alishukuru kwa juhudi zilizofanywa na wataalamu wa ukoaji migodini kwa kushirikiana na uongozi wa mgodi huo zilizofanikisha kuwaokoa.

Nyanga alisema wakiwa ndani ya shimo hilo, walikata tamaa ya kuiona dunia tena baada ya miili kudhoofika kwa kukosa chakula na maji na kupata hewa kidogo ya oksijeni kupitia miundombinu iliyokuwapo katika mashimo hayo.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Nyang'hwale, Dk. Princepius Mugishagwe, alisema hali za manusura hao sasa zinaendelea vizuri baada ya kupata huduma.

Akizungumza kwa niaba ya Shirikisho la Vyama vya Wachimba Madini (FEMATA), Mwenyekiti wa Chama cha Wachimbaji Madini Mkoa wa Geita (GEREMA), Misana Jeremeih, alisema tukio hilo linapaswa kuchukuliwa kama sehemu ya kujifunza kwa wachimbaji wadogo katika kujikinga na majanga.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Grace Kingalame, akizungumza kwa njia ya simu, alisema tayari wameweka utaratibu wa kuzuia wachimbaji kuingia katika mashimo yaliyofungwa.



Askari polisi akiwaondoa wafanyakazi na mafundi katika ujenzi wa jengo la ghorofa linalojengwa kwenye kiwanja namba 194 na 195 Kitalu 'U', Mtaa wa Rwagasole jijini Mwanza mapema wiki hii, baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Amos Makalla (hayupo pichani) kuamuru kusitishwa kwa ujenzi huo kwa kile alichokisema kuwa eneo hilo ni mali ya serikali na umilikishwaji wake ulighubikwa na ukiukwaji wa sheria. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Mke adaiwa kuua mume, watoto kwa kuwanyonga

**Na Ndalike Sonda,** BARIADI

JESHI la Polisi mkoani Simiyu linamsaka mkazi wa Kijiji cha Mwantemi, wilaya ya Itilima, ambaye hajafahamika majina kwa tuhuma za kuwanyonga hadi kufa, watoto wake wawili na mume wake, Bundu Ng'hambi (32). Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Kamishna Msaidizi (ACP) Edith Swai, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia juzi saa 7:00 usiku.

Alisema uchunguzi uliofanywa na jeshi hilo umebaini watoto wawili waliokuwa wamening'inizwa kwenye chumba wanacholala wazazi wao, dalili zinaonyesha wamefariki dunia kwa kunyongwa.

"Katika hali isiyo ya kawaida tulianza kuwapata watoto (hakutaja umri wao) waliokuwa wamening'inia kwenye chumba cha kulala wazazi wao lakini baadaye tuliona mwili wa baba yao nje ya nyumba walipokuwa wakiishi," alisema ACP Swai.

Kamanda huyo alisema mwili wa Ng'hambi ulikutwa ukiwa umening'inia juu ya mti mithili ya kujinyonga huku mke wa mwanaume huyo akitokomea kusikojulikana. "Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi wa tukio ili kubaini chanzo cha matukio haya, lakini tunaendelea kumtafuta mke wa marehemu ambaye mpaka sasa hajulikani alipo," alisema.

Kamanda Swai aliwataka wananchi mkoani hapa kutoa taarifa pale watakapomwona mwanamke huyo na akiwaita wote wanaojua kilichokuwa kikiendelea katika familia hiyo.

Swai alitoa wito kwa wananchi kutoa taarifa za migogoro ya kifamilia ili kupatiwa ufumbuzi kwa kushirikiana na serikali za vijiji au mitaa na viongozi wa kidini.

# Aliyedaiwa kuua mke, mwanafamilia mbaroni

**Na Steven William**
MUHEZA

JESHI la Polisi mkoani Tanga, linamshikilia Salehe Ally ambaye alikuwa anatafutwa kwa madai ya kuua mke na mwanafamilia kwa kuwakatakata na panga kisha kutoweka.

Tukio hilo lilitokea Julai, mwaka huu, katika kijiji cha Mkanyageni wilayani hapa, baada ya wanawake hao kwenda porini kuokota kuni.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Almachius Muchunguzi, alimwambia mwandishi wa habari hii jana kuwa mtuhumiwa huyo alikamatwa juzi mkoani Tabora na kurudishwa Tanga.

Waliouwawa siku hiyo ni Mwanahawa Hatibu ambaye ni mke wa mtuhumiwa na Sauda Sofiani ambaye ni mwanafamilia, ndugu wa mke wake.

Alisema mtuhumiwa huyo anajishughulisha na ufundi wa kufyatua matofali na ni mkazi wa kijiji cha Mkanyageni.

Kamanda Muchunguzi alisema kulingana na mahojiano na upelelezi uliofanyika, wamejiridhisha pasina shaka kwamba mtuhumiwa huyo ndiye aliyehusika na tukio hilo la mauaji ya wanawake hao.

Alisema mtuhumiwa huyo atafikishwa mahakamani baada ya upelelezi zaidi kukamilika.

Kamanda huyo ametoa wito kwa wananchi kufuata sheria na kutofanya makosa ya jinai kama ya kujichukulia sheria mkononi na watoe taarifa wanapoona uhalifu wa aina tofauti.

Akizungumza baada ya tukio hilo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Mkanyageni, Athumani Azacha, alisema baada ya kuupata mwili mmoja porini, wakati wakiutafuta wa pili, mtuhumiwa alipiga simu akiwa mafichoni akieleza kuwa Sauda naye wamemuua na maiti yake iko chini ya mkorosho na kuwataka waende kuichukua.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania wasikubali kuingizwa katika matukio ya uvunjifu amani

**KWA** takribani miezi miwili sasa, kumekuwa na kauli zinazotoka kwa wanasiasa wa chama tawala wakiwamo viongozi katika serikali, wapinzani na wananchi wa kawaida wakiwamo wanasheria ambazo zinaashiria uvunjifu wa amani, umoja na mshikamano ambao umetamalaki kwa zaidi ya miaka 60 sasa.

Baadhi ya kauli hizo, zimeibua hatari na ishara ya kuugawa Muungano wa Tanzania ulioasisiwa mwaka 1964 huku Zanzibar na Tanganyika zikitajwa hatua ambayo inaweza kuibua mgawanyiko katika pande mbili za nchi. Kauli hizo zinazoiweka nchi katika u-Tanganyika na u-Zanzibari zimeibuka baada ya kupitishwa kwa mkataba wa makubaliano (IGA) baina ya serikali ya Tanzania na kampuni ya DP World ya Dubai kwa ajili ya uendeshaji wa bandari.

Kauli iliyotolewa na mmoja wa wanasheria waliokuwa wakipinga mchakato huo, ilikuwa ya waziwazi na ya kibaguzi dhidi ya upande wa Muungamo huku ikimtuhumu hata kiongozi mkuu wa nchi kwamba anafanya hivyo kwa sababu hana uchungu na Tanganyika.

Baada ya kuhitimishwa kwa kesi iliyofunguliwa katika Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya ambayo jopo la majaji watatu lilibariki mkataba huo, baadhi ya wanasheria pia walijitokeza hadharani kuwa watavua majoho yao na kuingia barabarani kuwa watawashawishi wananchi waandamane pamoja nao.

Licha ya kauli hizo za wanasheria, wanasiasa pia wamekuwa wakipanda majukwaani na kutoa lugha za matusi na kejeli dhidi ya upande mmoja wa siasa au hata kwa viongozi wa serikali kwamba wanauza nchi kupitia mikataba wanayoingia. Licha ya kwamba wataandamana, baadhi ya watu hao wametamka hadharani kwamba watahakikisha Rais Samia Suluhu Hassan anaondolewa madarakani kabla ya kumaliza ngwe yake ya uongozi kwa awamu ya kwanza mwaka 2025.

Kwa jumla, kauli hizo hazina nia njema kwa ustawi wa taifa la Tanzania ambalo watu wake wanaishi kwa misingi ya umoja, amani na mshikamano na wamekuwa wakishirikiana katika masuala mbalimbali ya kijamii bila kubaguana kwa misingi ya udini, itikadi wala maeneo wanayotoka ikiwamo ukabila. Kwa hiyo kauli hizo zinapotolewa na watu wenye heshima kama wasomi, viongozi na wanasiasa, zinatia ukakasi na kuashiria mwisho usio mzuri kwa umoja wa taifa.


Hata hivyo, ni jambo la kufurahisha kwamba Mkuu wa Jeshi la Polisi, Inspekta Jenerali (IGP) Camillus Wambura, alitoa kauli juzi ya kuwaonya watu hao na kuwataka wasichokoze vitu vilivyolala. Wambura, bila kupepesa macho wala kuuma maneno, alitamka bayana kwamba watu hao wasithubutu kufanya mchezo huo kwa kuwa dola iko macho na watashughulikiwa ipasavyo kwa mujibu wa sheria.

Kauli hiyo ya IGP Wambura ni ya kupongezwa na imetolewa katika wakati mwafaka kuonyesha kuwa hakuna mtu aliye juu ya sheria na kwamba mtu au kikundi chochote kitakachothubutu kutaka kuipindua serikali hakitaonewa huruma bali kitashughulikiwa ipasavyo.

Pamoja na serikali kupitia Jeshi la Polisi kutoa onyo hilo, Watanzania kamwe wasikubali kuingizwa katika vitendo ambavyo vinaweza kusababisha machafuko ikiwamo umwagaji damu kwa wale watakaojaribu kuingia mtaaani. Kila binadamu ana uhuru wa kutoa mawazo na kufanya atakacho lakini hakuna kisicho na mipaka kwa maana kwamba sheria lazima zifuatwe.

Watanzania watambue kwamba panapotokea hali isiyo na usalama hakuna shughuli za maendeleo zitakazofanyika, hivyo matatizo ya kiuchumi na kijamii yataibuka ndani ya jamii na hatimaye watu kuingia katika umasikini. Nchi za jirani zilipitia mambo kama hayo na hilo liwe funzo kwa Watanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Msalaba Mwekundu mmeupiga mwingi elimu kukabili Marburg

**CHAMA** cha Msalaba Mwekundu Tanzania (TRCS) kilikuwa miongoni mwa wadau wa afya walioshirikiana na serikali kupambana na ugonjwa wa Marburg ulioibuka Bukoba, Kagera Machi mwaka huu.

Mwanzoni mwa Juni, mwaka huu, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alitangaza rasmi kuisha ugonjwa huo ambao ulisababisha vifo vya watu sita kutoka katika kata za Maruku na Kanyangereko mkoani Kagera.

Baada ya tangazo la kumalizika kwa ugonjwa huo, TRCS ilitumia wafanyakazi wa kujitolea waliopewa mafunzo kuelezea kwa wananchi jinsi ya kujikinga nao iwapo utaibuka tena.

Chama hicho kilifanya hivyo, kwa sababu kinaamini kwamba kuisha kwa ugonjwa huo haina maana hauwezi kurudi, ndipo kikaamua kuendelea na utoaji wa elimu kwa kutumia wafanyakazi 202 wa kujitolea.

Binafsi ninauchukulia uamuzi huo kama kuupiga mwingi, hasa kwa kuona mbali na kubaini kuwa wananchi hawana uelewa wa kutosha wa kupambana na Marburg na kuamua kuwapa elimu.

Kwa mujibu wa mratibu wa mambo ya huduma ya kwanza wa chama hicho, Kheri Issa, ni kwamba waliamua kubaki Bukoba kwa muda wa miezi mitatu kuanzia Machi hadi walipohitimisha mwishoni wa Julai, mwaka huu.

Elimu ambayo wananchi wameipata kupitia chama hicho ni kuzingatia suala la usafi wa mazingira, usafi wa maji, kunawa mikono kwa kutumia sabuni na vitakasa mikono, ambayo ilifanyika nyumba kwa nyumba.

Uamuzi wa chama hicho wa kushirikiana na serikali kuelimisha wananchi, unaweza kuwa umesaidia kuwajengea uelewa wa kutosha ili hata kama bahati mbaya utaibuka tena, watakuwa na mbinu za kujikinga.

Kubaki Bukoba na kutoa elimu, ninadhani ni mwendelezo wao wa kushirikiana na serikali katika matukio mbalimbali yanayoikumba jamii, yakiwamo ya ukame yaliyowahi kutokea nchini

Ukame ulisababisha watoto kukumbwa na utapiamlo, huku mifugo ikikosa maji na nyasi, hali inayosababisha ife na kuwafanya wakazi wa maeneo hayo kuwa katika mazingira magumu.

Kwa mfano, wamewahi kutoa msaada wa kibinadamu kwa waathiriwa wa ukame katika wilaya mbalimbali za mikoa ya Arusha na Manyara kwa kutoa vyakula, matunda, dawa na fedha taslim, ili angalau kupoza wananchi dhidi ya machungu yaliyotokana na ukame huo.

Ushiriki huo wa TRCS ni wazi kwamba wanatimiza wajibu wao vizuri wa kusaidiana na Wizara ya Afya, katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya utoaji wa elimu ya kuepuka majanga.

Inaelezwa kuwa chama hicho kilianzishwa ili kulinda masilahi ya afya ya binadamu, kuhakikisha heshima kwa hulka ya mwanadamu, kuzuia na kupunguza mateso ya kibinadamu, bila ubaguzi wowote kwa misingi ya utaifa, rangi, jinsia, imani za kidini, daraja la kijamii au maoni ya kisiasa.

Ninadhani kwa jinsi kinavyotimiza majukumu yake, jambo la msingi lingekuwa ni wananchi kukipa ushirikiano kwa kukubali kupata elimu ambayo inatolewa kwa lengo la kuwafanya Watanzania kuwa salama. Uwapo wao unaweza kuwa umesaidia kuondoa mtazamo wa baadhi ya watu waliokuwa wakiwaona wafanyakazi wa chama hicho wenye vikoti vyekundu vyenye alama ya msalaba na kudhani ni wanyonya damu.

Ingawa kwa sasa haisikiki sana kama zamani kuwa watu wa aina hiyo ni wanyonya damu, lakini inawezekana wapo watu wanaoamini hivyo, hasa wale wanaoishi maeneo ambayo ni mbali na mijini.

Lakini pia inawezekana kadri wanavyojikita karibu na wananchi na kuwapa elimu sahihi, hatua hiyo imesaidia kuondoa mtazamo huo potofu ambao ulikuwa unasababisha washindwe kupata huduma inayotakiwa.

Hivyo, ni vyema TRCS ikaendelea kujikita zaidi kwenye maeneo ya pembezoni hasa katika vijiji ambavyo bado wananchi wake hawajui chama hicho wala majukumu yake kwa jamii.

SAFU

FIKRA MBADALA

# Mahakama na Bunge visipotenda haki Watanzania sasa tupeleke wapi kilio?



Pascal Mayalla

LEO naendelea na makala kuhusu hii IGA ya DPW na bandari zetu jinsi inavyotusaidia. Hukumu ya kesi ya kupinga IGA imetoka na imebariki uhalali wa mkataba huu lakini bado naendelea kusisitiza, hoja zote za kisheria zilizoibuliwa na manguli wa kisheria, kukosoa mkataba huu, zijibiwe kisheria. Hukumu imejibu baadhi tu ya hoja, lakini hoja za manguli wakiwamo Chama cha Wanasheria wa Tanganyika (TLS) bado hazijajibiwa.

Mkataba huu unatoa funzo hata kwa Tanzania kwamba hata Zanzibar ina fursa ya kuingia mikataba ya kimataifa kama ilivyo Dubai ambayo iko chini ya Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE).

Kama mahakama imekubali kwamba japo Dubai si dola, lakini kupitia Montevideo Convention, mahakama imeona Dubai inakidhi vigezo kuingia kwenye mikataba ya kimataifa bila kuzingatia vigezo vya mikataba ya Lome na Geneva.

Kama ni hivyo, kwa nini Zanzibar hairuhusiwi kuingia mikataba ya kimataifa hadi idhaminiwe na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT)?

Kama Tanzania tunaweza kuingia mkataba wa kimataifa na Dubai ambayo si nchi, kwa nini Zanzibar izuiwe? Hii ni fursa kwa Zanzibar kuupanua uchumi wa buluu kwa kuanzisha bandari huru kama Japan, Dubai na Singapore ili nchi za Afrika zinunulie magari Zanzibar badala ya Japan na Dubai. Hili likifanyika, kila Mtanzania atakuwa na uwezo wa kumiliki gari.

Mjadala kuhusu hii IGA ya DPW una sura tatu, kihalisia, kisiasa na kisheria. Kihalisia, hapa nazungumzia vitu vya ukweli na uhalisia kabisa vilivyosababisha Tanzania ikaribishe DP World kutusaidia kuendesha bandari yetu.

Ni dhahiri kwamba bandari yetu ndio rasilimali muhimu na sehemu ya kimkakati kwa Afrika Mashariki kuhudumia eneo la maziwa makuu.

Hata hivyo, bandari yetu ya Dar es Salaam imeshindwa kutumia fursa hiyo kikamilifu kutokana na uwezo mdogo wa nchi yetu kiuchumi kuimarisha kiuwezo wa uendeshaji na kimitaji. Hiyo ndiyo sababu iliyofanya nchi yetu kutafuta mwekezaji wa kimkakati (strategic partner) wa kuungana nao, kutusaidia kuboresha uendeshaji ndipo akajitokeza DP World.

Hoja za kisheria ni kwamba kwa vile IGA ni suala la kisheria, nikiwa mwanasheria, niliweka hoja zangu mezani kuwa japo Bunge limeridhia DP World kuendesha bandari zetu, IGA ni makubaliano tu na si mkataba.

Kwa hiyo tukithibisha kuna matatizo, tunarekebisha kwenye mkataba wa HGA ili hii kazi nzuri ya Mama Samia, iendelee!"

Wanasheria nao wanajitokeza wakubwa kwa wadogo, vijana kwa wazee, wakiwamo manguli, wabobezi na wabobevu, wengine wakipinga mkataba huo kwa hoja za kisheria wakiwamo TLS na wengine wakiunga mkono.

Wiki hii mahakama imetoa majibu ya kisheria kwa hoja za kisheria kuhusu hii IGA kuwa iko sawa kwa sababu hii IGA imeleta maneno maneno na kelele nyingi.

Bado nashauri uwapo wa uwazi mkubwa na wa hali ya juu kwenye HGA ili mambo kama ya IGA ya bandari na DP World yasije yakajirudia.

Hii hukumu ya Mahakama Kuu kwenye hili la DP World na Bandari zetu, inaendelea kuthibitisha Tanzania tuna tatizo kubwa kwenye kitu kinachoitwa mgawanyo wa madaraka (sSeparation of powers), na 'checks and balances'. Serikali ikikosea inaweza kushtakiwa mahakamani na mahakamani ikaamua lakini Bunge letu tukufu likikosea na Mahakama ikikosea, hakuna pa kushtaki!

Katiba ndiyo sheria mama, hivyo sheria nyingine yoyote inayokwenda kinyume cha katiba ni batili. Serikali yetu imepeleka muswada wa sheria batili, Bunge likatunga sheria batili inayokwenda kinyume cha Katiba, Mahakama ikaitangaza ni sheria batili.

Serikali yetu badala ya kuibatilisha, ndiyo kwanza ikapeleka bungeni muswada wa mabadiliko ya Katiba kwa hati ya dharura na kuuchomekea ubatili huo ndani ya Katiba yetu. Mahakama Kuu ikasisitiza huo ni ubatili, Mahakama ya Rufani ikaubariki kwa hoja kuwa haiwezi kuliingilia Bunge!

Kama Bunge linaweza kupitisha madudu ya ajabu na Mahakama ikayabariki, Bunge na Mahakama visipowatendea haki Watanzania, Watanzania tukalilie wapi?

Niliwahi kuuliza kuhusu Bunge kujipendekeza kwa serikali, sasa nauliza je, Mahakama inaliogopa Bunge? Bunge na Mahakama vinaiangalia serikali, Bunge likifanya madudu, nani analiangalia?

Naomba nimalizie kwa kuzungumzia kidogo kitu kinachoitwa karma. Licha ya kelele zote zinazopigwa kuhusu IGA ya DP World na Bandari, Bunge limeziba masikio kwa mkuu wa mhimili huu kutoa kauli za kujimwambafai wakati serikali iko kimya bila kujibu hoja za kisheria zilizoibuliwa na watu na makundi mbalimbali wakiwamo TLS.

Naliomba Bunge na serikali yetu kujibu hoja. Pia niliiomba Mahakama kutenda haki. Kama uamuzi huu wa mahakama ni wa haki, sasa Watanzania hatuna budi bali kuheshimu uamuzi wa mahakama.

Serikali yetu, Bunge letu na Mahakama zetu zina wajibu wa kuwatendea haki Watanzania. Wajibu huo si hisani (favour) bali ni haki (right). Naendelea kusisitiza kwa Bunge letu, Serikali yetu na Mahakama zetu, hata kwenye hili la DP World na bandari yetu, Watanzania tutendewe haki na tusipowatendewa haki na vyombo hivi, lile lijamaa linaloitwa karma lipo na linaangalia!

**Wasalaam**
**Paskali**
**+255 754 270403**

MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Afadhali 'chawa wa Mama' wamemwagiwa majimoto



Na Joseph Kulangwa (kulangwasos@gmail.com)

MUNGU aliumba mbingu na nchi kabla ya viumbe wengine hai, wakiwamo binadamu, wanyama, ndege, samaki, wadudu na mimea na kumpa binadamu uwezo wa kuwasimamia na kuwadhibiti.

Lakini katika kujipatia riziki, viumbe hao walitegemeana kwa chakula, hivyo walikulana. Binadamu akala wote hao wengine, wanyama huku viumbe wengine hai waliosalia nao wakala wenzao mpaka binadamu wakajikuta wanaliwa.

Katika kudhibitiana, ikaonekana binadamu ana mamlaka zaidi dhidi ya wengine, hata kufikia wakati akaamua baadhi yao kuwafuga ili kuwapata kirahisi na kwa ukaribu zaidi. Ndio ukawa mwanzo wa mgawanyo wa wanyama wafugwao na wa porini.

Kwa hiyo wafugwao wakawa marafiki wa binadamu, ingawa kuna nyakati aliwageuza kitoweo. Lakini walionekana nao kuridhika pengine kutokana na walivyokuwa wakilelewa na binadamu na kuwa halali kuliwa.

Hivyo haikushangaza kumwona ng'ombe, kondoo, nguruwe, mbuzi, kuku au bata nyumbani kwa binadamu akifugwa, akila, kunywa na kulazwa kwenye kibanda au zizi.

Hata wasioliwa nao walionekana majumbani kwa shughuli maalumu za kazi na ulinzi. Mathalan, punda alikuwapo kwa ajili ya ubebaji na usafirishaji mizigo kama ambavyo mbwa alikuwa wa ajili ya ulinzi, huku paka akipambana na wanyama wadogo waharibifu kama panya.

Kwa upande wa wadudu, binadamu alipambana nao mwenyewe hata wale walioishi kwenye miili ya wanyama wafugwao, kama vile kupe na viroboto waliowaganda wanyama miilini.

Binadamu aliepuka sana kuishi na nyoka, nge, tandu, kunguni na chawa, kutokana na madhara yao, huku pia akimpenda na kumchukia nyuki kutokana na mazao yake ya asili-asali lakini pia hatari yake aking'ata.

Kama mtu alionekana kuwa na ukaribu na nyoka, tandu, mbu, kunguni, chawa na nge, wenzake walimshangaa na kumwona kama si binadamu wa kawaida au asiyejipenda.

Ndiyo maana ilipotokea mtu akaonekana akichezea nyoka au fisi, aliwekwa katika kundi la watu wa kushangaza na kutoaminika, ingawa baadaye ikazoeleka kuwa ni utamaduni kucheza nao katika vikundi.

Lakini aliyeonekana na chawa mwilini au nguoni au hata matandikoni, sawa na kunguni pia, alionekana mchafu na hakuwa na sababu ya kuchukuliwa vinginevyo. Ni mchafu basi hakuna jina lingine.

Na mtu wa aina hiyo alitengwa na kutakiwa kujisafisha kwa kuoga na sabuni lakini pia kufua nguo zake kwa maji moto kama si yenye dawa, ili kuondokana na wadudu hao wachafu wasababishao magonjwa pia.

Siku za karibuni katika nchi hii ya Nyerere, wakaibuka watu wakifurahia kujiita chawa. Wakaenda mbali na kujibatiza majina ya 'chawa wa Mama', wakafikia hatua hata ya kujisajili na wakasajiliwa hivyo!

Yakaibuka makundi kwa majina hayo kwa kasi ya ajabu, yakiamini kuungwa mkono na Watanzania, huku yakijinasibu kumwunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye siku moja kimaskhara akajikuta anayatamka kama kuyatambua vile.

Yawezekama Mama alidhani yana nia njema, lakini kumbe waliosoma kule naniliu, wakajua tu kuwa ni kujikomba kulikopitiliza kutaka kujisogeza karibu na Mama kwa maslahi binafsi, ya kutaka uongozi au ajira. Kumbe ni suala la Tumbo Street tu!

Juzi kati hapa tukasikia kuwa maji yamechemshwa na chawa wamemwagiwa kwa minajili ya kuwatokomeza ili kama kweli kuna watu wenye nia njema na Mama basi wajiite 'watetezi wa Mama'.

Lakini wajue watetezi wa Mama ni Watanzania wote kwa sababu Rais Samia ni Rais wa wote, aliyempigia kura John Magufuli na ambaye hakumpigia kura, kwani wote walikuwa chini ya wawili hao, Rais na Makamu ambaye alikuja kuwa Rais.

Tuwashukuru waliofikia uamuzi wa kuwasagilia mbali 'chawa' hao waliokuwa na nia ya kumnyonya 'damu' Mama yetu na kuvimba matumbo yao kwa kuvimbiwa, ingawa kiongozi wao anashikilia kuwa eti kwa kuwa wamesajiliwa waendelee na majukumu yao.

Nadhani waendelee na majukumu yao kwa kuwa chawa wa mawe au miti. Bila shaka uamuzi wa kuwamwagia majimoto ulizingatia chawa wenyewe ambao wamekwa wakijifanya hamnazo na kushabikia mambo yasiyo na kichwa wala miguu, ili mradi kuonekana wako karibu na mfumo!

Unashangaa dume zima na misharafa yake, kushadidia dume lingine kwa tambo na mbwembwe, ili mradi lina ukwasi na madaraka, kumbe kuna kitu linafukuzia ili liweze kuishi kwa utelezi wa ndizi Kitonga! Naipongeza CCM kwa kuachana na vikundi hivi vya 'chawa wa Mama'!

**Alamsiki!**

# Waziri ataka matumizi kliniki za ardhi

**Na Munir Shemweta,**
LUDEWA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk Angeline Mabula, amewaelekeza watumishi wa sekta ya ardhi nchini kuhakikisha wanakuwa na kliniki za ardhi kama ilivyoelekezwa na wizara ili kutatua changamoto za sekta ya ardhi.

Dk. Mabula alitoa maelekezo hayo juzi wilayani hapa mkoa wa Njombe baada ya kupokea malalamiko mbalimbali kuhusu changamoto za sekta ya ardhi katika mkutano wa hadhara akiwa katika ziara yake ya siku tatu mkoani Njombe.

Katika mkutano huo, wananchi walimlalamikia Waziri Mabula kuwa wamekuwa wakipata usumbufu kutoka kwa watendaji wa ardhi katika mambo mbalimbali yanayohusiana na sekta hiyo jambo linalowafanya kushindwa kupata huduma stahiki zikiwamo hatimilki.

"Wananchi wengi katika wilaya ya Ludewa hatuna hatimilki za ardhi.

Tukikosa hatimiliki maisha yetu yako hatarini maana tunaweza kunyang'anywa viwanja wakati wowote," alisema mkazi wa Ludewa, Cosmas Sanga.

Mkazi mwingine, Herman Luoga, alisema mbali na kupimiwa mashamba kwa ajili ya kupatiwa hati za kimila pamoja na kufuatilia mara kwa mara ofisi za ardhi katika Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa, wameshindwa kupata majibu hadi sasa.

Kutokana na malalamiko hayo, Waziri alisema: "Jambo ambalo ningependa watumishi wa sekta ya ardhi wafanye ni kuwa na klinik za ardhi ambazo wizara yake imeziekeleza kufanyika nchi nzima."

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, kupitia klinik za ardhi, watumishi wa sekta ya ardhi watatoka ofisini kwenda kwenye kata na kuweka vikao kwa ajili ya kusikiliza hoja, changamoto na kero kutoka kwa wananchi na wanaposikiliza lazima watoe majibu papo hapo kwa kuwa wao ndio wataalamu.

Alisema katika maeneo hayo wanaweza kukaa siku moja au mbili kutegemeana na uhitaji wa eneo husika na kuongeza kuwa kliniki hizo zinatakiwa kuzungukia kata zote za halmashauri. Alisisitiza kuwa watendaji hao kabla ya kwenda eneo husika lazima watangaze au kutoa taarifa mapema siku watakayokwenda.

"Kwa sababu wakati mwingine changamoto hakuna isipokuwa elimu. Mtu haelewi kwa nini amiliki ardhi kwa nyaraka.

Hajui akitaka kupimiwa aanzie wapi na mwingine amevamiwa katika eneo lake hajui afanye nini," alisema.

Dk. Mabula amemaliza ziara yake ya siku tatu mkoani Njombe baada ya kutembelea wilaya za Njombe, Makete na Ludewa. Mbali na kuzungumza na watumishi wa sekta ya ardhi na wananchi wa wilaya hizo, alikabidhi hatimilki kwa wananchi waliokamilisha taratibu za kupatiwa hati.



Mkurugenzi wa Bodi ya Sukari nchini, Prof. Kenneth Bengesi (katikati), akishirikiana na Balozi wa India nchini, Binaya Srikanta Pradhan (wapili kulia) na Meneja Mkuu wa Kitengo cha Uendeshaji Afrika na Kimataifa wa Mahindra, Sandresh Parab (wapili kushoto), kukata utepe kuzindua kituo cha mashine za kilimo (matrekta), jijini Dar es Salaam jana, chenye lengo la kukuza na kuendeleza sekta hiyo nchini, ili kukuza kilimo cha kisasa kwa gharama nafuu. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Sarga Motocorp, Sandeep Singh. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki zasisitizwa kupunguza riba kwa wachimbaji madini

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, amezitaka taasisi za kifedha kuangalia uwezekano wa kupunguza riba kwa wafanyabiashara ya madini ili kupata wateja wengi na kuruhusu wachimbaji wadogo kunufaika na mikopo hiyo.

Dk. Kiruswa aliyasema hayo juzi jijini Dar es Salaam wakati wa hafla ya kuwaaga wadau wa sekta ya madini wapatao 100 wanaotarajia kwenda China kwa ajili ya mafunzo.

Kundi hilo linahusisha wachimbaji wadogo na wa kati, wafanyabiashara, watoa huduma migodini, wataalam wa madini kutoka taasisi za wizara ya madini, taasisi za fedha ikiwamo Benki ya CRDB.

Waziri huyo aliwataka kuhakikisha safari hiyo inaleta matunda na wawekezaji wengi kwa kupata vifaa vya kisasa ili kuongeza uzalishaji wa madini.

Alisema ubalozi wa China kwa kushirikiana na Kampuni ya'Touchbroad ya nchi hiyo, imeandaa ziara hiyo ili kuwawezesha kukutana na wawekezaji wa madini nchini humo.

Pia alisema wadau hao watapata fursa ya kutembelea viwanda vya kutengeneza mitambo na vifaa vya uchimbaji na uchenjuaji pamoja na kuwawezesha kubadilishana uzoefu na wafanyabiashara wa madini nchini humo. "Niwaombe kila mmoja wenu akiwa China ahakikishe anatimiza malengo yake kadri anavyoweza ili ujuzi mtakaoupata uje kutusaidia kuboresha biashara zetu na kuongeza tija," alisema Dk. Kiruswa.

Naibu Katibu Mkuu Wizara hiyo, Msafiri Mbibo, aliwataka wachimbaji hao kutumia ziara hiyo kujifunza na kupata uzoefu pindi watakapotembelea viwanda vya kutengeneza mitambo na vifaa vya uchimbaji.

Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji wa Madini nchini (FEMATA), John Bina, alisema ziara hiyo itafungua milango ya nchi kuvutia wawekezaji wengi kwa kuwa ina sera nzuri katika uwekezaji.

Viongozi wengine walioshiriki ni pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Madini, Kheri Mahimbali, Mbunge wa Viti Maalum mkoa wa Iringa, Rita Kabati, Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Dk. Venence Mwasse, Mjumbe wa Bodi ya STAMICO, Lucas Seleli na wawakilishi CRDB.

# Ma-DED waagizwa kufuatilia ununuzi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewaagiza wakurugenzi wa halmashauri mkoani hapa kufuatilia ununuzi wa vifaa vya miradi ya shule badala ya kuwaachia walimu.

Ametaka suala hilo kutowaachia walimu kwa asilimia 100 kwa kuwa baadhi yao wameonyesha uzembe kutokana na kutosimamiwa.

Agizo hilo alilitoa jana baada ya kutembelea na kukagua ujenzi wa mabweni, madarasa na vyoo katika shule za sekondari za kidato cha tano zilizoko katika halmashauri za wilaya za Iramba, Ikungi na Singida ambazo mwezi Juni, mwaka huu, serikali ilitoa Sh. bilioni tatu ili zijengwe.

Serukamba alisema baadhi ya walimu ambao ndiyo wanaosimamia ujenzi wa shule hizo wameonekana kutokuwa na uharaka wa kuzijenga zikamilike.

Alisema kwa kuwa wameachiwa jukumu la kusimamia kwa asilimia 100 bila kufuatiliwa, wamesababisha vifaa vya ujenzi kutonunuliwa hadi sasa katika baadhi ya shule.

Akiwa katika Shule ya Sekondari Ndago ambayo kasi ya ujenzi wa mabweni imeonyesha kuwa ndogo, kiongozi huyo alimwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iramba na Mhandisi wafike shuleni hapo kufuatilia maendeleo ili ukamilike.

Pia aliwataka makandarasi ambao wamepewa zabuni za ujenzi wa shule hizo kuongeza idadi ya mafundi ili kasi ya kujenga madarasa na mabweni hayo iongezeke na kukamilika wiki inayoanza kesho.

Akiwa katika Shule ya Sekondari Ikungi, Serukamba alitoa siku tatu kwa viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi aliagiza hadi kesho kazi ya kuweka vigae katika mabweni ya shule hiyo iwe imekamilika.

Agizo hilo lilitokana baada ya kukuta mabweni na madarasa ambayo serikali ilitoa Sh. milioni 811.7 yamewekwa sakafu ya saruji badala ya vigae.

"Haiwezekani serikali imetoa fedha za ujenzi zikiwamo za kuweka vigae sakafuni lakini mmeweka sakafu ya saruji, nawaagiza wekeni vigae kesho (leo) jioni nitarudi kukagua ili Jumatatu nikabidhiwe mabweni rasmi," aliagiza.

# MAISHA

JUMAPILI AGOSTI 13, 2023

Nipashe

Baba, Mama na Mwana

Jumapili




Ukurasa 14

## Kula chapati laini



Ukurasa 14

## UREMBO:

Kucha fupi maridadi




## KATUNI

Ukurasa 16




# WAOW! UNAPENDEZA

Ukurasa 13

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA








| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| A | ■ | J | I | O | N | I |
| S | ■ | ■ | ■ | N | ■ | M |
| U | ■ | L | I | A | ■ | B |
| B | U | U | ■ | N | Z | I |
| U | ■ | G | O | A | ■ | S |
| H | ■ | H | ■ | ■ | ■ | H |
| I | N | A | M | A | ■ | A |

## AMSHA AKILI


HAYA, NGOJA TUONE LEO WANGAPI WANAZIJUA NAMBA ZA KIRUMI: UNGANISHA KUANZIA NAMBARI (i) MPAKA (ix) ILI KUKAMILISHA MCHORO.




## TOA TOFAUTI 5



## FUMBO TOTO




Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

MLA, MIA, JAA, NOA, KIAZI, AKOME, AMANA, JAMBO, CHIMBUA, IMKANDE

## WATOTO

# PAKA RANGI







Alichokifanya daktari

MTOTO Grace alikuwa akitembea juu ya sakafu ya marumaru kwa mwendo wa haraka, mama yake alimwangalia na huku akiwa na hofu asije akateleza na kuanguka chini.

Mama: Grace unakimbilia wapi, hujui kama unatembea kwenye marumaru?

Grace: Mama nakwenda kuchukua kitabu changu cha hadithi Juma ameniibia.

Mama: Lakini kuwa mwangalifu, usije ukaumia na mimi sina pesa ya kukupeleka hospitali.

Grace: Lakini mama kule shuleni mwalimu alitufundisha kwamba 'kuteleza si kuanguka', hivyo sina hofu.

Mama: Hapana mwanangu huo ni msemo tu alitaka kuwajenga muwe na ujasiri wa kufanya jambo ambalo awali umeshindwa.

**SWALI**

Taja aina tatu ya wanyama wa jamii ya swala wanaopatikana porini.

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Mama mkwe 'alininyang'anya' mume!

KARIBU tena msomaji wangu tuendelee na vimbwanga vyetu vya Maisha Ndivyo Yalivyo. Wiki kadhaa zilizopita nilijadili hapa maeneo mbalimbali yanayohusu wakwe na mikiki mikiki katika ndoa.

Kwa wale waliobahatika kusoma makala hizo wanaendelea kutoa uzoefu wao jinsi wanavyochukuliana na wakwe. Wanasimulia zaidi vituko vya wakwe katika ndoa zao.

Leo msomaji wangu nikupe simulizi ya dada mmoja ambaye ilibidi afungashe virago baada ya mama mkwe kuzidisha vituko, huku akiwa sambamba na kijana wake. Ilikuwaje?

Akasema hivi, mimi nina umri wa miaka 28. Nimebahatika kuzaa watoto wawili, wa kwanza wa kike umri miaka 12 na mwingine wa kiume umri miaka saba.

Nilikuwa nikiishi na mama yangu mzazi nikiwa mzaliwa wa pili. Tumezaliwa watatu, na kaka zangu. Nilikutana na kijana mmoja katika mizunguko yangu ya biashara, tukapendana.

Ikatokea nimepata ujauzito. Mama akawa mkali akaniuliza alipo mhusika nikamwambia ni mwenyeji wa kitongoji jirani na pale tunapoishi. Ndipo mama akaita ndugu zake wakanichukua kwenda kunikabidhi kwa yule kijana.

Kijana alinikubali kwa kuwa alikuwa ananipenda lakini mama mkwe alionyesha kutofurahia tukio lile. Huo ukawa mwanzo wa maisha mapya. Nakumbuka ndugu za mama mkwe walipopata habari zile walikuja na kumshauri tufungishwe ndoa ya kimila, jambo ambalo lilifanyika.

Niliendelea kuishi pale Mungu akanijalia nikajifungua mtoto wa kike salama. Mtoto alikuwa vizuri na afya njema. Kadiri nilivyoendelea kuishi pale afya ya mtoto ikawa haieleweki, usiku anaweweseka, na kuumwa mara kwa mara.

Kwa kushirikiana na mume wangu tukajenga nyumba nzuri eneo ambalo tulipewa jirani kabisa na nyumbani kwa mama mkwe. Nyumba ilipokuwa tayari, mama mkwe akaanza vituko. Kila siku lazima aje kwangu kutafuta chokochoko.

Kila siku anakuja na jipya la kunikwaza, nikimwambia mume wangu ananiambia nivumilie kwani ndivyo alivyo mama yake. Mtoto wangu ikafikia mahali akimuona mama mkwe analia sana au anamkimbia.

Niliposimulia hilo kwa baadhi ya majirani, wakanipa siri kwamba mama huyo ni mchawi na kwamba anaogopwa hapo kijijini na kwamba hata huyo mtoto wangu hayupo vizuri kwani amepumbazwa na mama mkwe wangu.

Nilipotafakari sana, siku moja nikamuaga mume wangu kwamba narudi nyumbani kwetu kwani vituko vya mama yake vimezidi. Nikamchukua mwanangu na vitu vyangu nikarudi kwa mama.

Nikaendelea kuwasiliana na mume wangu akanipa ujauzito mwingine nikazaa mtoto wa kiume. Mama akanipa eneo pale nyumbani nikajenga nyumba yangu ambako naishi na watoto wangu. Hivi sasa nachakarika nasomesha watoto wangu.

Baba watoto ni kama vile hatupo tena pamoja nimeamua kwenda Shinyanga kwa fursa za biashara, nina amani sina la kunikwaza tena. Wakwe wengi wanaharibu ndoa za watoto wao kwa ufinyu wa uelewa wa maisha yalivyo.

Mpenzi msomaji, hiyo ndiyo simulizi ya leo. Nikuongezee kidogo jinsi ya kuishi na wakwe ambao hawajaokoka. Yaani bado wanaendekeza nguvu za giza kuendesha maisha yao.

Mara utakapokuwa na wakwe ambao hawajaokoka, usifanye kosa la kuwahukumu matendo yao na misingi yako ya kidini. Kumbuka wanamhitaji Mungu na matendo yako ndiyo yanaweza kuwabadilisha.

Kumbuka siku zote kuwa mambo mengine wanayafanya kwa sababu ya kutokufahamu. Muombe Mungu akupe hekima ya namna ya kuchukuliana nao.

Unapokuwa nao waonyeshe tunda la roho la upendo ili uweze kuwavuta kwa Mungu. Kuwa makini kutokushiriki ibada zao za sanamu /miungu kama kutumia hirizi, madawa ya kienyeji, matambiko na kadhalika.

Kila mmoja wenu(wanandoa), anapaswa kuepuka mambo ambayo yanaweza kuharibu uhusiano wenu na awe na uwezo wa kuelezea pale anapoona wanaweza kuleta athari kwenye nyumba yao. Ila vyote hivi vifanyike kwa hekima.

Fanya maombi makali ya kuwaombea wakwe ambao hawajaokoka. Wasamehe pale wanapokosea, waonyeshe kuwa una Roho wa Mungu ndani yako.

Siku zote matendo yako yanapaswa kuwafanya wakwe zako kumuona Mungu aliye ndani yako na kwa kufanya hivyo anaweza kuambatana nawe kumfuata Mungu.

Hata hivyo, siyo kila mkwe utaweza kumvumilia. Mwingine hutengeneza mazingira mume wako akuchukie ili uondoke. Unajikuta mchana mama mkwe anakushambulia na mume akirejea usiku anakushambulia. Unakuwa huna mtetezi.

**Haya pia huwakuta wanaume. Fuatilia kituko hicho wiki ijayo. Ujumbe 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI

Na Godfrey Mushi

# Iko wapi ripoti uchunguzi matrekta ya Ursus?

BILA shaka Watanzania wengi wanakumbuka lile sakata la matrekta ya Ursus ambalo liliibua utata mkubwa hasa katika uwekezaji wake. Kilio kilikuwa kikubwa kila kona ya nchi.Bunge likaambiwa, likapokea na kulijadili.

Kana kwamba haitoshi likaunda kamati ndogo ya Wabunge na maofisa serikali kwenda kwa wananchi kuchunguza na kutoa majibu yake.

Sasa ni miezi minne imetimia hakuna majibu. Ingependeza kama serikali, ingelitoa majibu kabla ya Bunge kuwaumbua!

Hadi kufikia sasa, utata kuhusu madai ya kukiukwa kwa makubaliano ya mkataba wa mauzo ya matrekta kati ya Kampuni ya Ursus ya Poland na wakulima au wananchi wa Tanzania, unaacha maswali magumu ambayo kama hayatajibiwa kwa haraka, umma unaweza kujikuta ukiathiriwa na kupungua morali ya uzalishaji wa chakula na mazao ya biashara nchini.

Aprili 13, mwaka huu, Bunge lilielezwa kwamba tangu wakulima walipoingia mkataba na kampuni hiyo chini ya usimamizi wa Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC), hakuna vipuri vilivyoletwa nchini kwa mwaka wa pili sasa.

Taarifa ni kwamba walikubaliana na kampuni ya Ursus kwamba kwa miaka miwili wataendelea kupewa huduma ya vipuri, lakini matrekta hayo yamefika kwa wakulima na hakuna vipuri.

Baada ya kilio kusikika, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, aliamua kuipeleka Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji katika mikoa yenye malalamiko kwenda kusikiliza, kuchunguza malalamiko na changamoto za mkataba huo na kupeleka mapendekezo yake bungeni.

> **Kwa sababu inaelezwa kwamba wakulima ili kukabiliana na changamoto ya fedha za mkopo wa matrekta hayo, wanalazimika kununua na kutumia vipuri vya trekta, aina ya Massey Ferguson, kwa kuwa wenye matrekta hawana vipuri na wameshindwa kuvileta nchini.**

Kwa namna ambavyo mkataba huo ulivyogubikwa na utata, hata baada ya kamati kuwasilisha Bungeni mapendekezo yao kutokana na walichokibaini kwa wakulima kuhusu mkataba huo, kuna haja ya kuchukua hatua zaidi kwa kwa Bunge letu kuagiza, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kufanya ukaguzi wa kiuchunguzi, yaani 'forensic audit'.

Ndio! CAG anapaswa afanye forensic auditing katika mkataba huo ulioingiwa Oktoba 22, 2015 kati ya NDC na Ursus iliyojenga kiwanda cha kuunganisha matrekta hayo Kibaha mkoani Pwani kwa sababu kuna viashiria pia vya udanganyifu kama ambavyo malalamiko yametolewa na Mbunge Asia Halamga.

Kwa sababu inaelezwa kwamba wakulima ili kukabiliana na changamoto ya fedha za mkopo wa matrekta hayo, wanalazimika kununua na kutumia vipuri vya trekta, aina ya Massey Ferguson, kwa kuwa wenye matrekta hawana vipuri na wameshindwa kuvileta nchini.

Moja ya masharti ya mkataba huo, inaelezwa kwamba mkataba unawataka wawekezaji hao wanaolipwa kwa mkopo wa masharti nafuu, kujenga vituo vinane vya kukarabati matrekta na kuwa na magari ya kwenda vijijini kuhudumia matrekta ya wakulima.

Oktoba 27, 2014 huko Warsal, Poland. Rais wa Bodi ya Ursus, Karol Zarajczyk, alipokutana na Waziri Mkuu Mstaafu Mizengo Pinda (wakati huo Waziri Mkuu) pamoja na wafanyabiashara wenye nia ya kuwekeza Tanzania, alisema wako tayari kutoa mafunzo kwa vijana wa Tanzania waliopo vyuoni ili waweze kuunganisha matrekta hayo, kuyafanyia ukarabati na kutengeneza vipuri vyake wakati kunapokuwa na ulazima wa kufanya hivyo, lakini je hilo linafanyika?

Kwa muktadha huo, tunataka mabadiliko ya msingi ya mkataba, kati ya Tanzania na kampuni ya Ursus, ambayo kwa jinsi mkataba wao ulivyokaa, unapingana na mkataba mama ulioingiwa kuchukua mkopo kati ya Tanzania na Poland.

Haiwezekani tukaendelea kuliacha suala hilo kuchukua suara ya kisiasa, tuwasaidie wakulima wetu kwa kuzuia wasiuziwe matrekta mabovu.

• **Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com**



Kufunga ndoa katika ufukwe wa bahari au ziwa ni tukio la kipekee maishani, pichani ni baadhi ya harusi zilizofanyika katika maeneo hayo. **PICHA: PINTEREST**

MITINDO

Na Moshi Lusonzo



# WAOW! UNAPENDEZA

UKITAKA kupendeza zaidi kwa mwanamke ni lazima kuwa na chaguo zuri la mavazi ya kisasa.

Hata hivyo, inanogesha zaidi kama mavazi hayo yataambatana na mwendo maridadi na wenye madaha.

Pamoja na kupendeza kwa mavazi ya gharama, wanawake wengi wanashindwa kutembea vizuri hasa wakiwa kwenye mialiko ya sherehe mbalimbali.

Kama una mavazi mazuri na unahitaji kujiamini, ni lazima kujifunza namna ya kupiga hatua ukiwa na nguo yako muhimu.

**JIFUNZE KUTEMBEA**

Chagua vazi ambalo litakufanya utembee kwa madaha, mwendo wa pole au haraka lakini kwa muonekano mtulivu.

Hata kama limetengenezwa kwa aina tofauti ya vitambaa ni wazi unaweza kutembea kama inavyohitajika.

**VAA VIATU VINAVYOKUTOSHA.**

Kama unahitaji kuwa huru na raha zaidi katika mwendo, unatakiwa kuvaa viatu vyenye visigino vya wastani.

Ni vizuri viatu vya aina hiyo vitakupa usalama zaidi na muonekano mzuri. Ukitembea mwendo wa paka yaani kupishana miguu ni wazi utapendeza zaidi.

**MWENDO WA KINYONGA**

Unatakiwa kujifunza kwa ufasaha kutembea mwendo wa 'kinyonga' ukipiga hatua kwa kuhesabu. Ni muhimu mtu maalum akawa anakuangalia jinsi unavyotembea ili kukufanya uwe na mwendo unaotakiwa.

**KUWA HURU**

Unatakiwa kutulia katika siku yako hiyo muhimu, ukifanikiwa hilo kila kitu kwako kitakuwa rahisi. Usihofu kuhusu kutembea au jinsi ya kusimama bali fanya jambo hilo kama rahisi kwako na unaweza.





## UREMBO

Na Mary Geofrey

# Kucha fupi maridadi



KUKAA na kucha ndefu na huzihudumii vya kutosha ni kero na pia ni hatari kwa afya yako.

Huna haja kutumia mdomo kukata kucha kwani unaweza kusababisha bakteria kuingia mdomoni.

Katika safu hii leo tutaelekezana namna ya kutunza kucha zako kwa kuzikata kwa ufasaha.

Hatua za kufuata

Chukua kifaa chako cha kukatia kucha wembe sio mzuri sana.

Safisha kucha zako kwa maji ya moto mpaka ziwe laini kama unataka kula.

Anza kukata kucha kwa kuanza kidole cha pili baada ya kidole gumba.

Fuata mtiririko huo mpaka kidole kidogo na malizia na kidole gumba.

Usianze kukata kucha mkono wa kushoto anza wa kulia na hakikisha zoezi hili unalifanya kila baada ya wiki mbili, Hii ni muhimu sana usisahau nakuhakikishia hutaona kucha tena katika mwili wako.

Hatua hii ni muhimu kwa watu wote ili kuendelea kuonekana nadhifu wakati wote.



## MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Kula chapati laini

CHAPATI ni aina ya kitafunwa pendwa na watu wengi hasa maeneo ya pwani.

Hata hivyo, kuandaa kitafunwa hichi ni lazima ufahamu namna ya kukaanga ili iwe katika hali ya kuchambuka.

**Mahitaji**

Unga wa ngano vikombe vitatu, samli iliyoyeyuka vijiko vinne, chumvi kiasi chako na maji yasiokuwa moto wala baridi.

**Matayarisho**

Weka unga kwenye bakuli uchanganye na chumvi vizuri, weka samli uchanganye mpaka vidonge vyote viishe, weka maji kidogo kidogo ukiendelea kukanda unga mpaka ushikane na ulainike vizuri.

Funika unga kisha uweke pembeni kwa takriban dakika 30 au zaidi, funua unga wako utoe madonge matatu ambayo ukubwa wake itategemea na kibao chako cha kusukuma. Kama ni kikubwa unaweza hata ukafanya donge moja.

Sukuma donge moja moja kama chapati kisha upake mafuta na ukunje duara ili kufanya kuwe na matabaka na gawanya ukubwa unaotaka na ukunje vizuri chapati zako.



Ziache tena kwa takriban nusu saa au zaidi ili zizidi kulainika.

Ukimaliza bandika chuma cha kuchomea chapati jikoni na uache kishike moto.

Chuma kikiendelea kushika moto, sukuma chapati zako na weka kwenye kikaango uanze kuchoma.

Chapati ikishika rangi kidogo upande mmoja, geuza upande wa pili pia ishike rangi na weka samli upande mmoja.

Kaanga chapati kwa sekunde kadhaa huku ukiikandamiza chini kwa kitambaa au kijiko kikubwa ili ikolee rangi nzuri.

Geuza upande wa pili ufanye vivyo hivyo, kutumia mkono ama kifimbo cha chapati kunja chapati zako mara mbili na uzipige kwa juu.

Hapo chapati zipo tayari kuliwa na andaa zikiwa moto.

Mwisho

## MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya



# FAHAMU SABABU ZINAZOCHANGIA KUVUJA KWA NYUMBA

KUWA na nyumba bora na imara ni ndoto na furaha ya kila mtu anayemiliki au anayetarajia kumiliki nyumba hiyo.

Lakini inapokuwa kinyume cha matarajio ya kumiliki nyumba ya vigezo hivyo, moyo huinama japokuwa wakati mwingine hali hiyo inasababishwa na kukosea uchaguzi wa wataalamu wa ujenzi wa nyumba husika ambao hujenga chini ya kiwango.

Mtaalam wa masuala ya ujenzi, Andrew Kitale, anazungumzia sababu mbalimbali zinazochangia baadhi ya nyumba kuvuja muda mfupi baada ya ujenzi wake kukamilika.

Anasema kuna sababu mbalimbali zinazochangia nyumba nyingi kuvuja ambazo watu wanapaswa kuzifahamu na kuchukua hatua wanapojenga nyumba zao ili kuzuia athari za namna hiyo.

Kitale anasema miongoni mwa sababu kuu zinazochangia tatizo hilo ni pamoja na matumizi ya vifaa vya ujenzi vya hali ya chini ambavyo baadhi ya watu hufanya hivyo kwa kudhani kuwa wanaokoa pesa.

Sababu nyingine anasema baadhi ya vifaa vinavyotumiwa na mafundi wakati wa kuezeka huwa sio rafiki kwa paa na hivyo kudhoofisha kifuniko cha paa ambacho baadaye hutengeneza ufa na kupitisha maji.

Mbali na sababu hizo, pia anasema paa la nyumba linaweza kuharibiwa na upepo kama halikuezekwa kwa utaalamu mzuri, hivyo kuvuja.

Sababu nyingine anasema ni muundo wa paa lenyewe pamoja na makosa yaliyofanywa wakati wa kuezeka na kwamba kwa makosa hayo ya kuvuja kunaweza kutokea hata ndani ya mwaka mmoja baada ya ujenzi wa nyumba husika.

Nyingine, anasema ni ufungaji mbaya wa paa wakati wa kuezeka na kwamba kasoro kama hiyo huonekana haraka ndani ya wiki chache baada ya nyumba kuanza kutumika.

"Paa linaweza kuvuja kwa sababu ya ukiukaji wa matumizi ya teknolojia ya ujenzi. Kwa mfano, kitaalamu unatakiwa kuweka nyenzo za kuezekea katika tabaka tatu, wewe unaweka tofauti na hapo na makosa mengine madogo yanayofanana na hayo yanayofanywa wakati wa kuezeka," anasema.

Anashauri kwamba njia nyingine ya kuepuka paa kuvuja ni kuwa makini kuchagua wataalam wa kuezeka, kutumia vifaa bora bila kujali gharama, kufuata kanuni zote za uezekaji na kukagua paa la nyumba yako mara kwa mara angalau mara mbili kwa mwaka na kuondoa vitu vyote ambavyo hutuama juu yake ambavyo kwa namna moja ama nyingine hutengeneza nyufa hususani vyuma na vitu vizito.



## Yajue maajabu ya rangi 'smoke'



**Na Restuta James**

MSOMAJI mmoja alinipigia simu wiki iliyopita akitaka kujua kuhusu mpangilio wa sebule, akitaka kujua pia rangi inayopendekezwa na wataalamu wa mapambo ya ndani.

Pamoja na kwamba nilishaeleza kuhusu rangi, nimelazimika kuongeza jambo ambalo sikulizungumza wakati ule.

Mtaalamu wa mapambo, Ndigwako Asalile, anasema rangi zinazoshika kasi kwa sasa ni ile ile bluu tulivu (aqua blue), ambayo inaleta mwonekano wa kuvutia kama ikipakwa kwenye ukuta mkubwa na kuta ndogo zikapakwa 'smoke', kijivu na gardenia.

"Wapo wanaoamua kupaka kijivu iliyokoza (dark gray) na kijivu angavu (light gray), pamoja na gardenia. Huu ni mchanganyiko mzuri sana. Kwa wanaopenda rangi nyeupe nawashauri watumie 'smoke' ni nzuri zaidi," anasema.

Anasema rangi ya gardenia inafaa kupaka peke yake kwenye uzio au nje ya nyumba na kunakshi nguzo au vibaraza kwa rangi ya bluu tulivu.

**MPANGILIO WA SEBULE**

Hakikisha viti au sofa zako hazigusi ukuta, hii itakusaidia kuzuia kuchubua ukuta wako, pia mzunguko ndani ya nyumba. Hakikisha rangi inaendana na fanicha nyingine kama sofa, picha za ukutani, mapazia na taa. Hii inaongeza mvuto na utulivu ndani ya nyumba.

**Tuwasiliane kupitia restutajames@gmail.com na 0753333330**

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASI
BY ABDUL KINGO - 2023
SMS - 0713 447766
'USINIFATE!
KWA SABABU UMESHA'GOOGLE' UMEGUNDUA MIMI NAPELEKA UBUYU KWA MKEO KUHUSU FATUMA?
'MSIKIMBILIE SIASA HAKUNA KITU NI TABU TUPU NA KARAHA TELE! LAWAMA KILA KUKICHA! 'SIASA HAINA DILI' UTAKUFA MASIKINI
WEWE HUJAKWENDA ARUSHA KWENYE 'KONGAMANO' ULIKUWA TABATA KWA HAWALA!
AHAA! KWA HAWALA KUNA CHOO CHA NJE, HAKUNA FENSI
'UMBWA MAMBO?'
NIKIKUJIBU NIITE UMBWA NIPO PALE!
NIMESEMA NIKIKUJIBU'
UMESIMAMA MLANGONI KAMA JINI HUITI ABIRIA UNANIKERA UJUE...
NIITE ABIRIA WAKATI UNAENDESHA GARI UNAVIPITA VITUO KAMA UMEMUONA AFISA WA MKOPO WAKO WA 'KAUSHA DAMU'
MPE MPE!
MCHUPA BWANA! UNAWEZA KUKUTAWALA KULIKO NYUMBA NDOGO HUTAKI KUSIKIA IMEKUNUNIA!
NJAA INAWEZA KUKUFANYA UONEKANE MSONI, KUMBE!
SASA NIMESHA-PATA SOMO KWANINI MWANAUME AKIFA WANACHUNGUZA KOLOMELO 'NITA'GOOGLE'
MANENO YA WANAUME YANAHIFADHIWA KOONI, NDIO MAANA TUMEPEWA KOLOMELO LAKINI WANAWAKE HAWANA
*KINYUNYIZO CHA LEO...
KICHEKO CHA MWENYE NYUMBA AKIWA HAKUDAI KODI...

HABARI KIMATAIFA

# Odinga kuanzisha mgomo, wafuasi wake kukaa ndani

**NAIROBI,** KENYA

KIONGOZI wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga amesema wanaweza kuandaa maandamano ya raia kukaa majumbani ili kuepuka mauaji yanayofanywa na polisi.

Mkuu huyo wa muungano wa Azimio la Umoja, aliwaambia wananchi katika Kaunti ya Siaya, kuwa kuwaua watu kutoka nje ya nyumba zao ni sehemu ya kuzuia mauaji ya kikatili yanayofanywa na polisi pale raia wanapoamua kuandamana mitaani.

Alizungumza hayo wakati wa maombi ya madhehebu mbalimbali ya kuwaombea waathiriwa wa matumizi ya nguvu ya polisi.

Odinga alisema huenda muungano huo ukaamua kuwazuia wafuasi wake kutoka kwenye makazi yao.

Akitoa mfano wa matukio ya nyuma, aliishutumu serikali kwa kushambulia watu wasio na hatia na kujaribu kuzua hofu kwa kuwatumia polisi.

Alisema upinzani utawaelekeza wafuasi wake kukaa majumbani kama njia mbadala ya maandamano.

Kiongozi huyo wa upinzani alimlaumu Rais William Ruto na naibu wake Rigathi Gachagua kwa kusababisha mauaji yaliyothibitishwa na polisi, na aliongeza kwamba ubaguzi wa kikabila ulitumika hasa kwa kuwalenga jamii ambazo hazikuwapigia kura wakati wa Uchaguzi Mkuu wa 2022.

Odinga alisema kuwa Rais Ruto hakuwa amejitokeza hadharani kulaani vitendo hivyo vya polisi, badala yake aliwapongeza.

**BBC**



Meli ya Ocean Viking ikikaribia boti iliyobeba wahamiaji katika Bahari ya Mediterania hivi karibuni. **PICHA:IMAGO**

## Marekani iko tayari kutoa mafunzo marubani Ukraine

**WASHINGTON,** MAREKANI

MRATIBU wa Baraza la Usalama la Marekani, John Kirby amesema nchi yake iko tayari kuanza kutoa mafunzo kwa marubani wa Ukraine ya kurusha ndege za F-16 katika ardhi yake.

Kirby alisema hatua hiyo itachukuliwa endapo washirika wa Ulaya hawana rasilimali za kutosha kwa kutoa mafunzo.

"Ikiwa Ulaya haitaweza kutoa mafunzo, bila shaka, tuko tayari kuanza kutoa mafunzo kwa marubani wa Kiukreni hapa Marekani," Kirby alinukuliwa na CNN.

Wakati huo huo, alionya kwamba wakati Ukraine inapokea wapiganaji kutoka nchi za magharibi na kuunganishwa katika jeshi lake la anga, bado kuna safari ndefu hadi kufikia lengo.

"Sababu ya sisi kufanya hivi ni mapambano yetu ya muda mrefu na ya kuboresha uwezo wa kijeshi wa Ukraine kujilinda," aliongeza.

Kirby aliongeza kuwa pamoja na kuhamisha ndege na marubani wa mafunzo, washirika wa Ukraine pia wanapaswa kutengeneza vifaa vyote muhimu kwa ajili ya ukarabati na uendeshaji wa ndege za nchi za Magharibi.

Alibainisha kuwa yote lazima itachukua muda, na alithibitisha kuwa mafunzo hayo yanajumuisha pia lugha kwa marubani. CNN ilisema kuwa Marekani bado inasubiri washirika wa Ulaya kutoa mpango wa kuwafunza marubani wa Ukraine ndege za aina ya F-16.

Hata hivyo, kabla ya utekelezaji wa mafunzo hayo, bunge lazima liidhinishe rasmi mpango huu.

Hapo awali, Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky na maofisa wa Ulaya walisema marubani wa Ukraine wangepewa mafunzo mapema mwezi Agosti, lakini mpango huu hauonekani kama utatekelezwa.

Jana, gazeti la Washington Post, likiwanukuu maofisa wakuu wa serikali na jeshi la Ukraine, walisema kwamba kundi la kwanza la marubani sita wa Ukraine hawataweza kukamilisha mafunzo yao ya kuendesha ndege za F-16 hadi majira ya kiangazi yajayo.

Gazeti hilo lilinukuu kauli ya maofisa hao wakieleza marubani watalazimika kuchukua kozi za Kiingereza za miezi minne nchini Uingereza ili kujifunza istilahi zinazohusiana na upiganaji kwa kutumia ndege.

Wakati huo huo, wawakilishi wa serikali ya Ukraine walisema marubani hao tayari wanajua Kiingereza vizuri.

Mamlaka ya Ukraine inasisitiza kwamba nchi yao inapaswa kupokea ndege za kivita kutoka nchi za Ulaya haraka iwezekanavyo.

Lakini maofisa wa Marekani hawaamini kwamba ndege kama hizo zinaweza kusaidia katika mashambulizi ya sasa nchini Ukraine, liliripoti gazeti la Washington Post.

**BBC**

## Ecowas yapata kigugumizi kuivamia kijeshi Niger

**ABUJA,** NIGERIA

VIONGOZI wa mataifa ya Afrika Magharibi wamepata kigugumizi cha kutekeleza azimio la kuivamia Niger, badala yake wanatakafari zaidi hatua za kuchukua kuulazimisha utawala mpya kuachia madaraka.

Mipango yao ikiwemo tangazo la kuunda kikosi cha kijeshi kitakachokwenda kuivamia nchi hiyo, inatiwa ugumu kutokana na raia wengi wa Niger kuonekana kuunga mkono wanajeshi waliopindua serikali.

Juzi maelfu ya watu walimiminika kwenye mitaa ya mji mkuu wa Niger, Niamey kupinga maazimio ya Jumuiya ya Kikanda ya ECOWAS ya kutaka kuingilia kati kijeshi nchini humo.

Hadi jana ECOWAS bado haijafafanuwa kwa undani kuhusu kikosi hicho wala ratiba ya utekelezwaji wa maazimio hayo.

Hata hivyo, viongozi wa kanda hiyo walisikika wakisisitiza kuwa bado wanataka suluhisho la amani.

Mkutano muhimu wa kijeshi uliopangwa kufanyika juzi na jumuiya hiyo kwa ajili ya kujadili mapendekezo ya kuushughulikia mzozo wa Niger uliahirishwa kwa muda usiojulikana.

**DW**

## Meli yawaokoa wahamiaji 600 baharini

**ROMA,** ITALIA

MELI inayofanya operesheni za uokoaji kwenye bahari ya Mediterania inayoitwa Ocean Vking, imewaokoa wahamiaji 600 kwa muda wa saa 48 pekee.

Takwimu hizo zinaashiria kuwepo kwa ongezeko jipya la watu wanaofanya safari hatari ya kujaribu kuingia Ulaya.

Shirika linaloendesha meli hiyo la SOS Mediterranee, lilisema wengi wa watu waliookolewa walikuwa safarini kutoka mji wa mwambao wa Italia wa Sfax wakielekea kisiwa cha Lampedusa nchini Italia.

Kulingana na shirika hilo jumla ya watu 623 waliokuwa wakisafiri kwa kutumia boti hatari za mpira wamepatiwa msaada na sasa wamo kwenye meli ya Ocean Viking na wanatarajiwa kufikishwa kwenye bandari za Italia.

Wahamiaji hao ni kutoka mataifa ya Sudan, Guinea, Burkina Faso, Ivory Coast, Benin na Bangladesh.

Uokoaji huo umefanyika wiki moja tangu kutokea vifo vya makumi ya wahamiaji baada ya boti kadhaa kuzama baharini zikiwa njiani kuelekea mataifa ya Ulaya.

**DW**

MAKALA

# KUTOJIAMINI NA TAMAA ZA MADARAKA HUZAA UCHAWA



Na Magabilo Masambu

**Wako waliotamani kuwa mahakimu, walimu, polisi, wanajeshi, marubani lakini hawajawa. Tafsiri yake ni kwamba anayepanga uwe nani ni Mwenyezi Mungu, hivyo lazima uitazame nafasi uliyo nayo kama nafasi unayostahili japo bado unaweza kuendelea kufanya juhudi ufike ulikopangiwa kufika na si kuwa chawa.**

KUMEKUWA na wimbi la watu wanaojitokeza kuwa wasemaji wa baadhi ya watu mashuhuri au viongozi, machoni wakionekana watetezi wao mioyoni wakiwa na tamaa ya vitu mbalimbali.

Watu wanaosemewa na kusifiwa wanapaswa kuwa makini na watu hawa. Wasidhani wanawapenda sana bali wanapenda wanavyoweza kupata kutoka kwao. Tumejenga utamaduni wa kuona kila jambo linalofanyika ni jema lakini watu hawa hawa baadhi ya viongozi wakitoka madarakani, ndio watakuwa wa kwanza kusema walikuwa wanakosea.

Kutojiamini na tamaa za madaraka ni sababu mojawapo. Tabia hii hujenga woga na woga huleta hofu mwisho hakuna kitakachoweza kufanyika kwa kuamini kwamba huwezi kufanya hiki na kile na kwamba unahitaji fulani kukusaidia kufanikisha jambo lako. Sikatai kwamba ili kufanikisha mambo yetu tunawahitaji watu. Nafahamu kuna kutegemeana lakini iwe kwa haki. Si kupitia fitna na majungu kwa sababu ukiwa chawa maana yake kuna watu unawaumiza kwa kuwachongea, kuwafitinisha na kusema yasiyokuwapo ili mradi tu ufanikiwe.

Kutojiamini ni ugonjwa unaofifisha uwezo wa kufikiri. Badala yake kutakufanya ujipendekeze ili upate unachokusudia na zaidi kuyaona mambo kinyume kitu ambacho mara nyingi huwafanya watu wanaojua uwezo wako katika eneo fulani kushangazwa kama wewe ndiwe. Kuna watu wana elimu kubwa za vyuo vikuu lakini wameshidwa kuzitumia elimu hizo au kutumia uwezo wao mwingine wa vipawa walivyonavyo kutatua changamoto zao kwa kudhani kwamba kila wanachofikiri kufanya hakitakuwa sahihi kwao. Badala yake, wanaona njia rahisi ya kujipatia chochote ni kuwa chawa.

Kuna watu wanaamini kwamba mustakabali wa maisha yao uko mikononi mwa watu wengine na kwamba bila hao maisha yao hayapo. Lakini nataka ufikiri kwamba kama miongoni mwao hakuna aliyeamua uzaliwe kuna atakayeamua uwe nani? Wangapi katika maisha tumewahi kufikiri kuwa mtu fulani lakini hatujawa?

Leo hii kila mtu ukimuuliza atakwambia alitamani sana awe fulani. Wako waliotamani kuwa mahakimu, walimu, polisi, wanajeshi, marubani lakini hawajawa. Tafsiri yake ni kwamba anayepanga uwe nani ni Mwenyezi Mungu, hivyo lazima uitazame nafasi uliyo nayo kama nafasi unayostahili japo bado unaweza kuendelea kufanya juhudi ufike ulikopangiwa kufika na si kuwa chawa.

Wengi wasiojiamini na wenye tamaa, huwategemea sana wanadamu katika kutimiza malengo yao. Pale wanadamu hao wanapotoweka, watu hawa hubaki katika wakati mgumu maana imeandikwa: "Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu kuwa kinga yake na moyoni mwake amemwacha Bwana, maana atakuwa kama fukara nyikani palipo ukame, katika nchi ya chumvi isiyokaliwa na watu."

Sifa kubwa ya watu wasiojiamini wanakula na kuywa kwa kusifu watu waliofanikiwa au wanaodhani wanaweza kuwasaidia kupata kwa kuwa mahali Fulani. Nchini kwetu kwenye eneo la siasa na uongozi, hili limeonekana zaidi katika kutafuta madaraka. Lazima ufike wakati tutakaoweza kuamini kwamba, tunaweza kuendesha maisha yetu bila madaraka ya kisiasa labda iwe imeandikwa na kama ndivyo bado hakuna atakayeweza kukwamisha hilo, bali akipatikana atakuwa na nafasi ya kuchelewesha tu.

Hatari yake ni kwamba wale wanaosifiwa wakijiingiza kwenye mtego huu wa kuamini kwamba sifa hizo wanazistahili, maana yake taifa litapata viongozi wasio na uwezo au wenye uwezo watakaokuwa tayari kutoutumia uwezo wao kwa hofu ya kupoteza nafasi za madaraka, hivyo nyekundu kusema ni nyeupe huku wakiona ni nyekundu.

"Bwana wa majeshi ameapa akisema hakika yangu kama vile nilivyoazimia ndivyo itakavyokuwa na kama nilivyokusudia ndivyo itakavyotokea" (Isaya 14:24). Ibrahim na Sara katika uzee wao wakapata mtoto kwa sababu ahadi ya Mungu ilikuwa palepale pamoja na kwamba Ibrahimu alijaribiwa akazaa na kijakazi. Hata hivyo, bado jaribio hilo halikuzuia ahadi ya Mungu.

Tunao mfano halisi leo kwamba Nelson Mandela alifungwa miaka 27 gerezani lakini bado kusudi la Mungu la kuwa Rais wa kwanza mweusi Afrika Kusini likawa palepale. Hofu ya nini, nani aliyewahi kufikiri kwamba iko siku Tanzania itapata Rais mwanamke? Lakini leo tunaye na mambo mengine yatakuwa hivyo.

Kwa hiyo kuna mambo mengi ya kujifunza na kuondoa hali ya kutojiamini badala yake tufanye yale tunayoona yako sahihi kwa wakati sahihi bila kutegemea watu wengine watufanikishie ndoto zetu. Ukijiamini utakuwa na uwezo wa kujaribu kufanya mengi na katika hayo mengi, utajikuta njia zako za mafanikio zimo humo humo.

Wengi tunashindwa kufanikiwa kwa kutojaribu kwa sababu hatujiamini, hivyo tumo kifungoni ingali tunatembea. Tukiacha uchawa taifa litakuwa salama kwa sababu tutakuwa na uwezo wa kuyaona makosa, hivyo kusema hapa tunakosea na pale tunapatia.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Kwaheri Kalenga Nzazi Vivi wa Les Mangelepa, mtunzi wa 'Embakassy'*



Na Adam Fungamwango

**Watanzania hasa wale wa miaka ya nyuma, wanamfahamu mwanamuziki huyo kwani aliingia nchini akiwa bendi ya Orchestre Baba National iliyokuwa ikiongozwa na Baba Gaston Ilunga wa Ilunga, ambayo ilitunga na kuimba wimbo wa 'Kakolele Viva Christmas', uliosumbua sana na hadi leo hupigwa siku kadhaa kabla ya sikukuu hiyo ya Noeli.**

EMBAKASSY ninakwenda oooh moyo, natizama juu chini ooo Mola aaa..." Ni moja ya mashairi machache ya kiswahili yaliyomo kwenye wimbo huo uitwao 'Embakassy' uliopigwa na bendi ya Orchestra Les Mangelepa yenye maskani yake Kenya, albamu yake ikifyatuliwa mwaka 1978.

Embakassy ni jina la Uwanja wa Ndege nchini Kenya miaka ya nyuma kabla ya kubadilishwa baadaye na kuitwa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Jomo Kenyatta, ikiwa ni kumbukumbu ya Rais wa Kwanza wa nchi hiyo, Mzee Jomo Kenyatta.

Habari kutoka Kenya zinasema mtunzi wa wimbo huo, Kalenga Nzazi 'Vivi', amefariki dunia. Gazeti la Daily Nation la Kenya limeandika kuwa mwanamuziki huyo alifariki dunia Jumatano iliyopita asubuhi jijini Nairobi.

Kiongozi wa bendi hiyo, Kabila Kabanze 'Evani', aliliambia gazeti hilo kuwa ni pigo kubwa kwa bendi yao na mashabiki wa muziki Afrika Mashariki na Kati kwa ujumla, akisema walikuwa kwenye maandalizi ya kutoa albamu yake.

Kabila alisema Vivi alikuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa moyo huku familia yake ikisema alianguka nyumbani kwake na kufariki dunia dakika chache baadaye na mwili wake kwenda kuhifadhiwa kwenye Hospitali ya Mama Lucy, jijini humo.

Baadhi ya wanamuziki wakaliambia gazeti hilo kuwa walikutana kwa ajili mazoezi lakini mwenzao hakutokea.

"Na kila tukipiga simu haipokewi mpaka mchana na tukatuma baadhi ya watu nyumbani kwake wakakuta taarifa hiyo ya kusikitisha," alisema meneja wa bendi, Geoge Ouma Jojo.

Vivi amefariki dunia akiwa na miaka 70 na ameitumikia bendi ya Les Mangelepa kwa miaka 47, akiwa mmoja wa waanzilishi.

Watanzania hasa wale wa miaka ya nyuma, wanamfahamu mwanamuziki huyo kwani aliingia nchini akiwa bendi ya Orchestre Baba National iliyokuwa ikiongozwa na Baba Gaston Ilunga wa Ilunga, ambayo ilitunga na kuimba wimbo wa 'Kakolele Viva Christmas', uliosumbua sana na hadi leo hupigwa siku kadhaa kabla ya sikukuu hiyo ya Noeli.

Vivi aliimba sauti ya kwanza kwenye wimbo huo na ndiye aliyekuwa akiimba kwenye nyimbo zote za Baba Gaston na Les Mangelepa pia.

Baba Gaston aliyezaliwa Lubumbashi, Jimbo la Shaba, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (zamani Zaire), ndiye aliyewaingiza Vivi na Kabila kwenye bendi yake hiyo aliyoianzisha. Mwaka 1971 iliamua kuondoka Zaire na kufanya ziara Tanzania ambapo ilipiga kwenye kumbi kadhaa kiasi cha miaka minne hivi na kujipatia umaarufu mkubwa kabla ya mwaka 1975 kwenda Kenya ambako iliamua kuweka makazi yake huko.

Mwaka 1976, robo tatu ya wanamuziki akiwemo Vivi, walimkimbia Baba Gaston na kuanzisha bendi waliyoiita Les Mangelepa. Mwaka 1978 walitoa albamu ambayo ndiyo iliyowatambulisha na kuifanya bendi hiyo si kuwa kubwa tu, bali kuheshimika Afrika Mashariki na Kati nzima, iliyoitwa 'Embakassy.'

Vivi ndiye aliyetunga kibao hicho kilichobeba albamu nzima, maudhui ya wimbo huo ni kwamba alikuwa anamuaga mpenzi wake Suzzy aliyekuwa akisafiri kwa ndege.

Vivi alikuwa anamuombea afike salama na maneno mengi ya mapenzi, wakiwa kwenye Uwanja wa Embakassy Kenya, ambapo pia aliusifia uwanja huo.

Ni wimbo ambao ulisababisha kuna wakati wapate udhamini kutoka Shirika la Ndege la Kenya kwa kuzitangaza ndege zake na uwanja pia.

Kwenye albamu hiyo kulikuwa na nyimbo zingine kama 'Maindusa', 'Mimba', 'Nyako Konya.'

Baada ya kuwa bendi tishio ilifyatua vibao vingine kama 'Sakina', 'Walter', Amua', na vingine vingi ambavyo vyote marehemu aliimba sauti ya kwanza na kutunga pia.

Wanamuziki waliounda bendi ya Les Mangelepa, Bwamy Walumona 'Le capitaine', ambaye ndiye alikuwa kiongozi wa bendi wakati huo, Kabila Kabanze 'Evani', Kelenga Nzazi 'Vivi' mwenyewe na Babibanga wa Tshilumba 'Kai Kai'.

Wengine ni Lutulu Kaniki 'Macky', Kasongo Fundi 'Petit Jean', Lukangika Maindusa 'Moustang', Mwepe Mutshi 'Cavalou', Lumwanga Mayombo 'Ambassador',Tabu Ngongo Idelphonce, Mukala Wa Mulumba 'Bebe', Tshimanga Zadios, Twikala Wa Twikale 'Petit Pierre', Kabe Kimambe na Kabebe Mukangwa 'Picolo.'

Mipango na mazishi ya mwanamuziki Vivi inapangwa na familia, ndugu na jamaa, ikiwemo uongozi wa bendi ya Les Mangelepa ambayo hadi leo bado ipo.

Mungu amumweke mahali pema peponi mtunzi wa Embakassy, Kalenga Nzazi 'Vivi.'

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

CAROLINA, binti mrembo, aliyeumbwa akaumbika, mwenyewe anajiita Carry. Akifahamu fika jinsi alivyo mzuri na kubabaisha kila mwanaume anayekutana naye barabarani, anageuka kuwa mtu mwenye kiburi, jeuri, dharau na majivuno kwa watu. Atamsalimia yule tu aliyempenda kumsalimia. Ataongea na mtu atakayemchagua na si kila mtu. Anaweza kuziba hata pua akipita mtu ambaye yeye anaona si wa hadhi yake. Si mwanaume wala mwanamke. Jirani na anapoishi, kuna kijana mgeni asiyepungua miaka 25 hivi aliyehamia hivi karibu eneo la Kinondoni Moscow. Anaitwa James.

# Kafie kwenu-6

Alikuwa kijana anayeishi maisha ya hali ya chini, akipanga chumba kimoja. Jicho lake naye liliona urembo wa Carry. Akaamua kujaribu. Kilichompata hatosahau maishani mwake. Fuatilia hadithi hii ya kusikitisha, kuhuzunisha, kufurahisha, kuburudisha na kufundisha kwa wakati mmoja.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

NGOJA nikwambie kitu, wewe ni mwanamke mrembo sasa, naamini ni wanaume wengi wanakupenda na wenye uwezo kuliko mimi...."

"Wenye pesa zao na mali zao, ongezea hilo." Akamkatisha.

"Ni kweli nafahamu hilo."

"Enhee, sasa mbona unajitia uhayawani!"

"Siku zote mapenzi na pesa ni vitu tofauti. Mapenzi yanatakiwa kwanza yaanze halafu pesa inarutubisha, lakini pesa haiwezi kuanzisha mapenzi..."

"Naona siku hizi we bwana umekuwa mtunzi mzuri wa nyimbo, tafuta mfadhili au mdhamini akupeleke studio, utatoka rafiki yangu ili uondokane na hali uliyonayo."

"Narudia vile vile kukwambia Carry kuwa nakupenda."

"Koma wee usiniletee uchuro hapa. Kwanza ishakuwa mkosi, na safari yangu niliyoipanga kwenda siendi tena, naweza kupata majanga makubwa kuliko haya, ngoja nirudi zangu tu nyumbani."

"Poa, kwaheri Carry."

Hakujibiwa.

Akaondoka kwa hasira kurejea nyumbani. Hasira zake hazikuwa moyoni tu, hata alivyokuwa anatembea alionekana hivyo.

Alisahau pozi zake za kutembea kwa madaha kama twiga.

Bado James aliendelea kumtazama hadi akipopotea kwa kukata kona kwenye njia inayoelekea kwao.

******************************

Mwezi mmoja ulipita. Hali ya afya ya James ikaanza kuzorota. Alijihisi mchovu, hamu ya chakula mdomoni ilimuondoka kabisa.

Ikasababisha nguvu kupungua mwilini, hivyo akapunguza kufanya kazi ambazo alikuwa akizifanya awali.

Ikamsabishia kupungua hata kile kipato kidogo ambacho alikuwa anakipata. Akaamua kwenda zahanati ya karibu kupima ili kujua ni kitu gani kinamsibu.

Vipimo vilionyesha kuwa ana ugonjwa wa malaria pamoja na UTI. Pesa ya matibabu ikawa tatizo. Alichomudu ni ya vipimo tu.

Akawaambia madaktari na manesi kuwa alikuja na pesa za vipimo tu, hivyo wampe muda akatafute ya matibabu.

Akaondoka taratibu, kichwani akiwaza jinsi gani ataipata pesa ya matibabu, mwili ukiwa hauna nguvu kutokana na ugonjwa na njaa.




Ilikuwa ni saa saba mchana, jua kali. James alikuwa akitoka maeneo ya Kinondoni A, akirejea nyumbani kwake Kinondoni Moscow.

Alitembea taratibu mno na kuna sehemu alisimama au kukaa chini kabisa. Ni maeneo yenye kivuli cha mti au nyumba yenye baraza.

Mwisho kabisa aliamua kukaa kwenye moja ya magurudumu lililochimbiwa ardhini na kubaki nusu, kwenye mti mmoja mkubwa uliotengeneza kivuli kinachovutia watu wengi kupumzika na kufanya biashara.

Akiwa kwenye lindi la mawazo, ghafla aliona bajaj iliyokata kona na kushuka chini kidogo kwenye barabara ya mavumbi ikipunguza mwendo.

Akaipuuzia na kuendelea mapumziko yake, ili kukusanya upya nguvu kabla ya kujikongoja kwenda nyumbani.

"Wewe kaka unaitwa kwenye bajaj ileee."

Sekunde chache zilizopita alikuwa akiiangalia lakini akaipotezea akihangaika na yake, akasikia anaitwa aende kwenye bajaj hiyo hiyo.

Kwanza alishangaa, siyo kawaida kuitwa na mtu yeyote mwenye uwezo wa kukodi bajaj ili kumpa lifti.

Labda akodishiwe wakati anakwenda kununua vitu vya kufanyia kazi kama kujenga, au vibarua vingine.

Kwa mbali aliona dereva ametoa kichwa na kumwangalia.

"Njoo unaitwa." Sauti ya mwendeshaji ilimwita.

> **Angeweza kuwaambia waende tu kwani ilionekana kama anawachelewesha, lakini kwa sababu ilisimama kwa ajili yake, alijikongoja mpaka akafika.**

Alinyanyuka kivivu, akitembea taratibu, akijivutavuta ikionyesha kabisa hayupo vizuri kiafya.

Angeweza kuwaambia waende tu kwani ilionekana kama anawachelewesha, lakini kwa sababu ilisimama kwa ajili yake, alijikongoja mpaka akafika.

Hamu yake kwanza ilitaka kumjua ni nani aliyesimamisha bajaj kwa ajili yake?"

"Unaitwa na abiria ndani." Mwendesha bodaboda akaonyesha kuwa kuna mtu nyuma amtazame.

Akapatwa na mshtuko mkubwa. Hakutegemea kukutana na mtu kama yule.

"Carry?" akajiuliza mwenyewe.

"Panda twende, si unakwenda nyumbani." Ilikuwa ni sauti nyingine kabisa, tofauti ya alivyoizoea.

Njaa, kuchoka na jua kwa pamoja vilimfanya asiweze kumtambua vema.

Akapanda kwenye bajaj na kumuangalia kwa makini ndipo alipogundua kuwa siyo yeye.

"Vipi James mbona hivyo, umepatwa na nini?"

"Hapana, niko sawa tu, nimechoka."

"Hapana bwana, pamoja na kwamba sijakuzoea sana, lakini hiyo siyo sauti yako."

"Hamna kitu."

"Kuna kitu James, haupo hivi, umepatwa na nini?"

"Aaah, naumwa Catty."

"Nini tena James?"

"Malaria na UTI."

"Umekwenda kupima hospitali wamekwambia hivyo au unahisi tu?"

"Ndiyo nimetoka zahanati kupima nimeambiwa hivyo."

"Sasa umepata matibabu?"

"Mhhh! Dada yangu we sijui nikwambie nini. Nilikuwa na pesa ya kupima tu, ya matibabu sikuwa nayo, hivyo narudi nijitafutetafute ili niende nikapate sindano na dawa."

"Lini?"

"Siku yoyote ile Catty?"

"Na ugonjwa unakusubiri tu?"

"Sasa nitafanyaje, pesa sina na nina wiki sasa sifanya kazi yoyote kwa sababu ya kusikia vibaya, maana hata nguvu ya kufanya kazi nilikuwa sina." Akaongea kwa sauti ya chini, ya kukata tamaa na aibu pia.

Muuliza maswali hakuuliza swali lingine lolote kitu kilichoendelea na muulizwaji akaa kimya.

Bajaj ilisimama mita kadhaa kutoka kwa kina Catty.

Waliteremka, baada ya kulipa pesa alimwambia mwendesha bajaj kuwa atampigia tena baadaye.

Catty aliongozana taratibu na James hadi nje ya nyumba yao ambayo ilikuwa na geti.

Wakati James akiandaa maneno yatakayotumika kuagana na Catty pamoja na shukrani zake alishtushwa na sauti na msichana huyo.

"Hebu njoo ndani kwanza tuongee." Akashangaa. Kwa muda mfupi tu tangu akutane naye akaona yupo tofauti na dada yake.

Akataka kukataa lakini ukarimu aliofanyiwa, kupewa lifti, na kutakiwa kuingia ndani huku akijua kwa hali aliyonayo hawezi kupewa kazi yoyote ile ya kuifanya, akakubali. Akajua huenda kuna jambo lingine. Labda chakula.

Akakaribishwa varandani na kushuhudia hali halisi ya nyumba ya wanawake warembo jinsi ilivyo.

Ilipambwa kwa mapambo mbalimbali ya kisasa, makochi, meza, viti, meza ya kulia chakula, shefu ya kuweka viatu na vitu vingine vingi vilivyomshangaza na kumfurahisha.

Kukaribishwa na mwanamke mrembo kama yule, tena varandani na siyo nje kwa mtu kama yeye ambaye amekuwa akiandamwa na matukio ya unyanyapaa, ilimfariji kwa kiasi kikubwa.

Wakati akiwa amesimama akishangaa uzuri na ndani humo pamoja na nakshi za taa, akakaribishwa kwenye kochi.

"Kaa kwenye kochi James unasimama mtu mgonjwa kama wewe, utaanguka..."

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# HAMISA AMHURUMIA MTOTO WAKE

HATIMAYE mwanamuziki na mwanamitindo Hamisa Mobeto, amewataka watu kuacha kumjadili mtoto wake vibaya kwani inaweza kumuathiri kiakili.

Mobeto, amesema hayo baada ya kuulizwa na waandishi wa habari kuhusu utata unaozingira kuhusu baba wa mtoto huyo ambaye inajulikana ni wa mwanamuziki Diamond.

"Nisingependa kumuongelea mtoto wangu kwa sababu ni mwanangu wa miaka sita anakua na kuna vitu ataviona. Nafikiri kwa mtoto, hilo si jambo zuri kwa ukuaji wake wa afya ya akili au kitu chochote, na pia sidhani kama ina kitu chochote cha kujielezea, nadhani muda wa kujielezea ulishapita," Hamisa alisema.

Mrembo huyo mama wa watoto wawili, amesema kwamba kitendo cha Diamond kukaa kimya siku ya kuzaliwa kwa mwanawe wala hakijawahi kumpa msongo wa mawazo, kwani anaamini yote ni mipango ya Mungu.

# MSANII MR P ACHUKIZWA KUIVAMIA NIGER

MWIMBAJI wa Nigeria kutoka kundi lililokuwa likiitwa P-Square, Peter Okoye, maarufu kama Mr P, ameelezea kuchukizwa kwake kwa Jumuiya ya Kiuchumi ya Afrika Magharibi, ECOWAS, kuazimia kutumia nguvu nchini Niger.

Akijibu kupitia ukurasa wake wa Twitter, Mr P alishutumu jumuiya hiyo kwenda kupigana na Waafrika wenzao.

"Afrika inaungana na magharibi kupigana na Waafrika wenzao ni jambo la kuchukiza," amesema.



## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**CHELSEA YAPANDA DAU**
CHELSEA iko tayari kuongeza ofa yao kwa kiungo wa kati wa Brighton, Moises Caicedo, baada ya Liverpool kuwasilisha dau la pauni milioni 111 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ecuador mwenye umri wa miaka 21. **(Guardian)**

**LAVIA AKARIBIA CHELSEA**
CHELSEA inakaribia kukubaliana na kiungo wa kati wa Southampton mwenye umri wa miaka 19, Romeo Lavia wakati wakijaribu kumsajili nyota huyo raia wa Ubelgiji. **(Star)**

**LIVERPOOL, CHELSEA VITANI**
LIVERPOOL bado inamtaka Romeo Lavia, na wanatarajiwa kufanya mazungumzo zaidi na Southampton kuhusu mchezaji huyo ambaye anawindwa pia na Chelsea. (Sky Sport)

**USAJILI WA ADAMS WAKWAMA**
HATUA ya Chelsea kutaka kumleta kiungo wa kati wa Marekani mwenye umri wa miaka 24, Tyler Adams, kutoka Leeds United kwa dau la pauni milioni 20 imekwama. **(Sky Sport)**

**CITY YAMKOMALIA PAQUETA**
MANCHESTER City inajiandaa kuwasilisha ombi jingine la kumsajili kiungo wa kati wa West Ham, Lucas Paqueta, baada ya kuwa na ofa ya awali ya pauni milioni 70 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil mwenye umri wa miaka 25 kukataliwa. **(Football)**

**CANCELO KUTUA CITY**
MLINZI wa Manchester City, Joao Cancelo, amerejea katika orodha ya wachezaji wanaosakwa na Barcelona, huku wakala wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno mwenye umri wa miaka 29 akijaribu kupangua mpango huo**. (Sport)**

**VILLA YAMFUATA ZANIOLO**
KLABU ya Aston Villa inasubiri jibu kutoka kwa Galatasaray baada ya kutoa ofa ambayo inajumuisha ada ya mkopo ya euro milioni tatu na chaguo la euro milioni 20 la kumnunua kiungo wa kati wa Italia, Nicolo Zaniolo, mwenye umri wa miaka 24. **(Fabrizio Romano)**

**TOMIYASU SOKONI RASMI**
ARSENAL imeweka bei ya pauni milioni 30 kwa mlinzi wa Japan mwenye umri wa miaka 24, Takehiro Tomiyasu, ambaye anamendewa pia na klabu ya Inter Milan. **(Mail)**

**HAMMER KUTUA SHEFFIELD**
KLABU ya Sheffield United imekubali ada ya pauni milioni 15 kumsajili kiungo wa kati wa Coventry City, raia wa Brazil mwenye umri wa miaka 26, Gustavo Hamer. **(Telegraph)**

**DOKU KUMRITHI MAHREZ**
KLABU ya Manchester City inamfikiria mshambuliaji wa Stade Rennais na Ubelgiji, Jeremy Doku, mwenye umri wa miaka 21, kama mbadala wa winga wa Algeria, Riyad Mahrez (32), ambaye amejiunga na Al-Ahli. **(Telegraph)**

**RAMSEY ANUKIA BURNLEY**
KLABU ya Burnley imekubali ada ya pauni milioni 14 ili kumsajili kiungo mshambuliaji wa England, Aaron Ramsey, mwenye umri wa miaka 20 kutoka Aston Villa, ambaye wamewekewa kipengele cha kumnunua tena kwenye mkataba huo. **(Sports)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# CITY KUMKOSA TENA KIUNGO DE BRUYNE

●●●Ni baada ya kuumia tena pale pale kama ilivyokuwa katika...

**LONDON, England**

PEP Guardiola amesema anatarajia Kevin De Bruyne atakuwa nje kwa "wiki" baada ya kiungo huyo wa Manchester City kupata jeraha tena ambalo lilikatiza fainali yake ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

De Bruyne alilazimika kutoka nje kwa tatizo la msuli wa paja katika kipindi cha kwanza cha ushindi dhidi ya Inter Milan mjini Istanbul Juni, mwaka huu na akatolewa tena mapema wakati wa mechi ya ufunguzi ya Ligi Kuu England dhidi ya Burnley iliyochezwa juzi usiku.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 alibadilishwa baada ya dakika 23 tu ya ushindi wa mabao 3-0 pale kwenye Uwanja wa Turf Moor na nafasi yake kuchukuliwa na Mateo Kovacic.

"Alijeruhiwa tena kwa bahati mbaya," alisema Guardiola.

"Sehemu na nafasi sawa na Ligi ya Mabingwa Ulaya na atakuwa nje kwa muda. Inategemea ukubwa wa jeraha, lakini atakuwa nje kwa wiki chache."

Licha ya kuwa na miezi miwili pekee kati ya fainali ya Ligi ya Mabingwa na kuanza kwa msimu wa Ligi Kuu England, Guardiola alisisitiza De Bruyne alijiona yuko sawa vya kutosha kuanza dhidi ya Burnley.

"Alikuwa sawa, alipambana sana," alisema Guardiola.

"Alijisikia vizuri sana. Labda lilikuwa kosa langu kumwanzisha lakini anapojeruhiwa baada ya dakika 15 au 20 si kitu kibaya. Inapofika baada ya dakika sita ni uchovu wa misuli, inabidi tuzungumze na madaktari."

SportPesa | LIVE IN PLA

MECHI KALI
CHELSEA
VERSUS
LIVERPOOL
1 | 2.76
X | 3.51
2 | 2.49

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MESSI AIPELEKA MIAMI NUSU FAINALI




**NEW YORK, Marekani**

LIONEL Messi alidumisha rekodi yake ya kufunga katika kila mechi akiwa na Inter Miami FC wakati timu yake mpya ilipotinga hatua ya nusu fainali ya Kombe la Ligi kwa ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Charlotte FC, mchezo uliofanyika Fort Lauderdale, Florida, juzi.

Bao la nane la Messi katika mechi tano tangu kuwasili kwake lilipatikana zikiwa zimesalia dakika nne pekee na huku Miami wakiwa tayari wamefunga magoli matatu mbele ya mashabiki 22,000 waliohudhuria kwenye Uwanja wa DRV PNK.

Miami itasafiri kumenyana na mabingwa wa mwaka jana wa Eastern Conference, Philadelphia Union keshokutwa huku wakitafuta kuendeleza mabadiliko yao ya ajabu tangu kumkaribisha mshindi huyo mara saba wa tuzo ya Ballon d'Or.

Josef Martínez aliifungia Miami bao la ufunguzi dakika ya 12 kwa penalti, huku goli la pili likipatikana dakika ya 30.

Mbio za Messi kwenye eneo la penalti ziliwapa wakati mgumu walinzi wengi wa Charlotte, huku mchezaji wa kimataifa wa Marekani, DeAndre Yedlin akitumia vizuri pasi ya ya Robert Taylor kufyatua shuti kali kutoka katikati ya eneo la hatari la kufunga la tatu.

"Unapokuwa na Messi, unajua anahitaji tu nafasi. Anahitaji sekunde moja," alisema Kocha wa Charlotte, Christian Lattanzio, mara baada ya mchezo huo.

"Lazima uwe mkali sana kumzuia asitoe uchawi ambao amekuwa akitoa tangu alipokwenda Barcelona alipokuwa na umri wa miaka 16."

Pengine hakuna mchezaji aliyenawiri zaidi tangu kuwasili kwa Messi kama Taylor. Baada ya kufunga mabao matano katika mechi 52 za MLS kabla ya Messi, kiungo huyo wa Finland ana mabao manne katika mechi tano akiwa na nyota huyo wa Argentina.

# United yamuuza Fred Fenerbahce

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER United imekubaliana na Fenerbahce kumuuza kiungo wa kati wa Brazil, Fred, klabu hizo zimethibitisha.

Klabu hiyo ya Uturuki iamefikia makubaliano ya kimsingi yenye thamani ya euro milioni 10 pamoja na nyongeza ya euro milioni tano.

Fred jana alipaa kwenda jijini Istanbul ili kufanyiwa vipimo vya afya na tayari maslahi binafsi yamefikiwa.

Fred aliambiwa na Kocha, Erik ten Hag wakati wa majira ya joto hayupo katika chaguo lake baada ya kuwasili kwa, Mason Mount kutoka Chelsea.

Alikosa ziara ya kujiandaa na msimu mpya nchini Marekani baada ya kupewa muda wa kushughulikia masuala yake kibinafsi.

Kulikuwa na nia ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 kutoka Fulham, Galatasaray na klabu za Saudi Pro League, lakini yeye ameamua kwenda Fenerbahce baada ya kukubaliana ada na United.

Fred aliwasili Old Trafford mwaka 2018 chini ya kocha wa zamani Jose Mourinho kwa uhamisho wa pauni milioni 47 kutoka Shakhtar Donetsk na anaondoka akiwa amecheza mechi 213 ndani ya misimu mitano, akifunga mabao 14.



CHEZA USHINDE KASINO

# KITAYOSCE RASMI TABORA UNITED, YASAJILI WAPYA 12

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Kitayosce itakayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kwa mara ya kwanza msimu huu, rasmi sasa itaitwa Tabora United FC, baada ya kukamilisha taratibu zote za mabadiliko ya jina, imeelezwa.

Klabu hiyo ambayo hata kwenye ratiba iliyotolewa na Bodi ya Ligi ilikuwa inaendelea kujulikana kama Kitayosce ilitoa taarifa jana wamekamilisha taratibu zote za kisheria.

"Uongozi wa klabu unayofuraha kuufahamisha umma na wapenda soka Tanzania na nje ya nchi kuwa leo (juzi)Agosti 11, 2023 rasmi timu yetu imebadilishwa jina na mamlaka husika zinazosimamia mchezo wa soka nchini kutoka Kitayosce na kuwa Tabora United Football Club.

Mabadiliko hata yamefuata hatua zote za kisheria na kiutaratibu na yanalenga kuboresha uendeshaji wa klabu.



Ahsanteni kwa ushirikiano mliotupa katika kipindi chote cha Ligi Daraja la Kwanza (Ligi ya Championship), na ni matumaini yetu tutakuwa pamoja zaidi kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara 2023/24," iliandika taarifa rasmi ya klabu hiyo.

Wakati huo huo klabu Tabora United imemnasa kocha zamani wa makipa wa Yanga, Razack Siwa (pichani), kwa ajili ya kuboresha benchi lao la ufundi.

Klabu hiyo imesajili wachezaji wapya 12, ambao ni Shaffih Mohamed kutoka Nzega United, Maurice Reuben (Mbuni FC), Abdallah Madirisha (Biashara United), Aron Kalambo (Polisi Tanzania), Abbas Nziajose (Taifa Jang'ombe), Kelvin Igendelezi (Polisi Tanzania), John Noble, Mutuale Nyongani (Maniema DRC), Lumiere Kalumba (TP Mazembe), Andy Bikoko, Toauya Jean Didie ( Rajaa FC-Burundi) na Kelvin Pemba wa Mbabane Swallows ya Eswatini.

# Simba, Yanga hesabu mezani

INATOKA UK. 24

na mechi nyingine kwa sababu hiyo ni 'dabi' na inaangaliwa nchi nzima pamoja na nchi za jirani.

"Najua ni itakuwa 'dabi' na sio vita, ukiwa kwenye mpira lazima utakutana na mechi kama hizi, mechi zinazohusisha timu kubwa katika nchi, sitokuwa na presha yoyote kwa sababu pamoja hii ni mechi yangu ya kwanza ya dabi hapaTanzania, nina uzoefu wa mechi hizi, nimewahi kucheza mechi kubwa kama hizi huko nilipotoka," alisema Gamondi.

Alisema ni furaha kwake kukutana na Simba kwa sababu anajua ni timu kubwa kama ilivyo Yanga, lakini wapo watakaolia na watakaofurahi baada ya mpira kumalizika.

Beki wa kati wa Yanga, Dickson Job, alisema yeye na wachezaji wenzake wanaitaka mechi hiyo ili kuendeleza furaha kwa mashabiki wao ambao wamewaunga mkono tangu msimu uliopita.

"Wachezaji wote tuko tayari na tunaitaka hii mechi, tumefanya maandalizi mazuri na tunasubiri muda ufike ili tukawape furaha mashabiki wetu," alisema Job.

Wakati huo huo, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Kamishna Msaidizi, Almanchius Mchunguzi, alisema kuelekea mchezo huo wameimarisha ulinzi kwa ajili ya usalama wa watu na mali zao.

Mchunguzi alisema anafahamu mchezo wa leo utakusanya watu wengi na kwa sababu hiyo Jeshi la Polisi limeongeza ulinzi zaidi ili kuhakikisha kila kitu kinaenda sawa.

"Niwataarifu tu wananchi, ulinzi umeimarishwa zaidi, watu watatazama mpira na kuondoka salama wao na mali zao, kwa wale ambao watataka kutumia wingi wa watu na uwepo wa mchezo wa kesho (leo) kufanya matukio ya uhalifu wasithubutu, wataishia kwenye mikono yetu," alisema Mchunguzi.

# Azam, Singida kujiuliza

INATOKA UK. 24

raia wa Brazil katika mchezo uliopita, Bruno Gomes, kwa sababu hakuwa katika maandalizi ya muda mrefu lakini ana imani atakuwepo kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Naye Kocha Mkuu wa Azam, Youssouph Dabo, amesema mchezo wa leo ni muhimu kwao kwa ajili ya kuwarejesha wachezaji kwenye morali baada ya kupoteza mechi iliyopita dhidi ya Yanga.

Dabo alisema ameyaona na ameyafanyia kazi mapungufu yaliyowagharibu, hivyo wanatarajia kupata ushindi katika mechi ya leo na si matokeo mengine tofauti.

"Wachezaji wangu wako tayari kwa ajili ya kutafuta ushindi kesho (leo), nina imani tutafanya vizuri, kwangu michuano hii ni mizuri kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa Ligi Kuu, kila mechi inanipa kitu cha kufanyia kazi, kwa maandalizi tuliyoyafanya ni matumaini ya ushindi, hatutarudia makosa ya mchezo uliopita" alisema Dabo.




SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAPILI - 13/08/2023

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 3367 | Chungnam Asan vs Cheongju FC | 1.84 | 3.28 | 3.84 |
| 13:15 | 5629 | NEC Nijmegen vs SBV Excelsior | 1.49 | 4.28 | 5.37 |
| 14:00 | 1040 | Brest vs Lens | 3.91 | 3.50 | 1.97 |
| 14:00 | 5092 | Aberdeen vs Celtic | 7.15 | 5.16 | 1.33 |
| 14:30 | 4849 | St Truiden vs Anderlecht | 3.13 | 3.33 | 2.15 |
| 15:00 | 1046 | Dinamo Moscow vs Baltika Kaliningrad | 1.66 | 3.80 | 4.42 |
| 15:00 | 2559 | Randers vs Nordsjalland | 3.31 | 3.61 | 2.02 |
| 15:00 | 2609 | Vejle BK vs Midtjylland | 3.61 | 3.51 | 1.95 |
| 15:15 | 4092 | FC Basel vs Lausanne-Sport | 1.60 | 4.12 | 4.63 |
| 15:30 | 4076 | AZ Alkmaar vs GO Ahead Eagles | 1.33 | 4.85 | 7.72 |
| 15:30 | 5124 | Feyenoord vs Fortuna Sittard | 1.13 | 7.53 | 13.87 |
| 16:00 | 1503 | Nantes vs Toulouse | 2.57 | 3.40 | 2.73 |
| 16:00 | 1554 | Ilves Tampere vs KuPS Kuopio | 3.64 | 3.13 | 1.94 |
| 16:00 | 3221 | IFK Goteborg vs Djurgardens IF | 3.29 | 3.29 | 1.99 |
| 16:00 | 5306 | Brentford vs Tottenham | 2.72 | 3.60 | 2.47 |
| 16:00 | 5434 | Clermont Foot vs Monaco | 3.35 | 3.60 | 2.11 |
| 16:00 | 5705 | Montpellier vs Le Havre | 1.92 | 3.50 | 4.12 |
| 17:00 | 1090 | Motherwell vs Hibernian | 2.74 | 3.24 | 2.43 |
| 17:00 | 2780 | Hearts vs Kilmarnock | 1.79 | 3.63 | 3.98 |
| 17:00 | 4526 | Cercle Brugge vs Racing Genk | 2.93 | 3.53 | 2.17 |
| 17:00 | 4752 | Brondby vs Lyngby | 1.77 | 3.66 | 4.21 |
| 17:00 | 5000 | Eupen vs Brugge | 4.89 | 3.99 | 1.59 |
| 17:30 | 2421 | Zenit St Petersburg vs Fakel | 1.35 | 4.63 | 7.61 |
| 17:30 | 3515 | FC Luzern vs BSC Young Boys | 3.50 | 3.65 | 1.90 |
| 17:30 | 5904 | FC Lugano vs Yverdon-Sport FC | 1.39 | 4.64 | 6.60 |
| 17:45 | 3245 | Almere City vs Twente | 4.95 | 4.16 | 1.54 |
| 18:00 | 1185 | Celta Vigo vs Osasuna | 2.13 | 3.25 | 3.66 |
| 18:00 | 3796 | SCR Altach vs WSG Wattens | 2.49 | 3.24 | 2.51 |
| 18:00 | 4328 | RB Salzburg vs Austria Vienna | 1.37 | 4.64 | 6.05 |
| 18:00 | 4507 | Rapid Vienna vs TSV Hartberg | 1.53 | 4.02 | 4.83 |
| 18:00 | 5595 | Lillestrom vs Viking | 2.25 | 3.56 | 2.78 |
| 18:00 | 5901 | Aalesunds vs Ham-Kam | 2.10 | 3.51 | 3.10 |
| 18:05 | 2177 | Rennes vs Metz | 1.50 | 4.32 | 6.54 |
| 18:30 | 4715 | Hammarby vs Elfsborg | 2.82 | 3.33 | 2.20 |
| 18:30 | 5345 | BK Hacken vs Varbergs Bois | 1.23 | 5.45 | 8.69 |
| 18:30 | 5480 | Chelsea vs Liverpool | 2.76 | 3.51 | 2.49 |
| 19:00 | 4104 | Aarhus vs Silkeborg | 1.73 | 3.62 | 4.53 |
| 19:15 | 5561 | Sivasspor vs Samsunspor | 2.06 | 3.47 | 3.21 |
| 19:30 | 1194 | Charleroi vs Standard Liege | 2.04 | 3.49 | 3.24 |
| 20:00 | 2819 | CSKA Moscow vs Sochi | 1.55 | 3.86 | 5.35 |
| 20:15 | 2906 | KVC Westerlo vs KAA Gent | 3.38 | 3.63 | 1.95 |
| 20:15 | 5969 | Valerenga vs Haugesund | 1.70 | 3.76 | 4.33 |
| 20:30 | 2112 | Derry City vs Drogheda Utd | 1.50 | 3.93 | 5.25 |
| 20:30 | 2161 | Villarreal vs Betis | 1.78 | 3.91 | 4.32 |
| 21:45 | 1412 | Fenerbahce vs Gaziantep BB | 1.36 | 4.79 | 7.10 |
| 21:45 | 1697 | Strasbourg vs Lyon | 2.62 | 3.59 | 2.57 |
| 21:45 | 2538 | Adana Demirspor vs Caykur Rizespor | 1.59 | 3.98 | 4.86 |
| 22:05 | 4147 | Hajduk Split vs Slaven Belupo | 1.25 | 5.03 | 9.06 |
| 22:30 | 1309 | Getafe vs Barcelona | 5.83 | 3.74 | 1.64 |
| 22:30 | 3325 | FC Arouca vs GD Estoril | 2.07 | 3.18 | 3.48 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumapili Agosti 13, 2023
Nipashe



## City kumkosa tena De Bruyne

UKURASA 21



Aziz Ki

Kibu Denis

# Azam, Singida FG kujiuliza

**Na Mwandishi Wetu, TANGA**

KOCHA Mkuu wa Singida Fountain Gate, Hans van der Pluijm, amesema atatumia mchezo wa kutafuta mshindi watatu wa Ngao ya Jamii dhidi ya Azam FC kusahihisha mapungufu aliyoyaona kwenye mchezo uliopita alipokutana na Simba.

Pluijm alisema lengo lao kwanza kabla ya kuanza kwa michuano hiyo ilikuwa ni kutwaa Ngao ya Jamii msimu huu lakini walishindwa na sasa anahitaji kumaliza vizuri mashindano hayo.

"Tumetoka kwenye lengo la kuchukua Ngao ya Jamii msimu huu, lakini bado haitufanyi tuudharau mchezo dhidi ya Azam FC, tumewaona wakicheza na Yanga ni timu nzuri, lakini kwa mazoezi ya siku mbili tuliyofanya nina imani na timu yangu itafanikiwa kushika nafasi ya tatu," alisema Pluijm.

Alipongeza vijana wake wako katika hali nzuri na tayari kiufundi wamejiandaa kwa kuonyesha mbinu mpya lakini wakicheza kwa nidhamu kwa sababu wanahitaji kumaliza katika nafasi ya tatu.

"Tumekuja kushinda sio kushiriki, tumepoteza dhidi ya Simba, sasa tunaenda kukutana na Azam FC, vijana wako vizuri, tutacheza kwa nidhamu ya juu ili kufikia malengo yetu ya sasa ambayo angalau kupata ushindi wa tatu," alisema Pluijm.

Aliongeza alishindwa kumtumia nyota wake

INAENDELEA UK 23

# SIMBA, YANGA HESABU MEZANI

## ●●●Makocha wafurahia kukutana, waahidi 'Samba' litaonyeshwa...

**Faustine Feliciane na Saada Akida, TANGA**

TAJI la kwanza kwa msimu mpya wa mwaka 2023/24 linatarajiwa kuchukuliwa wakati watani wa jadi nchini, Simba na Yanga watakapokutana katika mechi ya hatua ya fainali ya kuwania Ngao ya Jamii itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani ,jijini hapa.

Yanga ambao ndio mabingwa watetezi wa taji hilo ndio ilikuwa ya kwanza kutinga fainali ya michuano hiyo baada ya kuichapa Azam FC mabao 2-0 wakati Simba iliwafunga Singida Fountain Gate FC penalti 4-2, kutokana na kutoka suluhu ndani ya dakika 90 za kawaida.

Fainali hiyo itachezwa kuanzia saa 1:00 usiku na itatanguliwa na mchezo wa kusaka mshindi wa tatu ambao utawakutanisha Azam dhidi ya Singida Fountain Gate kuanzia saa 9:00 mchana, kwenye uwanja huo huo.

Simba itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-0 walioupata mara ya mwisho timu hizo zilipokutana katika mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kuelekea mechi hiyo, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho' na Miguel Gamondi, Kocha Mkuu wa Yanga, kila mmoja amejinasibu wapo tayari na wanafahamu umuhimu, changamoto na ugumu wa 'dabi' hiyo.

Robertinho alisema timu yake inapenda kuchezea mpira na amekuwa muumini wa kuchezea mpira kwa kuanzisha mashambulizi kutoka nyuma lakini ameandaa mbinu nyingine tofauti kwa ajili ya mchezo wa leo.

Alisema kila mchezaji katika timu yake ameonyesha nia ya kutekeleza majukumu na anaamini wataonyesha kiwango bora kitakachowafanya wafikie malengo.

"Kila mchezaji wangu anajua majukumu yake ikiwamo safu ya ushambuliaji, na sitaki kuwapa presha kwa sababu najua umuhimu wa mchezo wa kesho (leo) kwa soka na ushabiki wa Tanzania, utakuwa mchezo mzuri sana, na burudani itaonekana kwa upande wa timu yetu kutokana na aina ya uchezaji wetu," alisema Robertinho.

Kocha huyo alisema haangalii upya wa benchi la ufundi la wapinzani wake na anachokifanya yeye ni kukijenga kikosi chake na kuandaa mbinu za kuwapa ushindi.

"Tuko tayari na kamili kwa ajili ya mechi hiyo, najua Simba itakachohitaji, tumejipanga kila idara, tayari nimeandaa mbinu zitakazosaidia kutupa matokeo mazuri, tuko tayari," Robertinho alisema.

Kauli hiyo iliungwa mkono na mchezaji wake, Israel Mwenda, ambaye alisema wachezaji wote wapo tayari kwa mchezo wa leo na wanataka kuwapa furaha mashabiki wao.

"Tumejiandaa vizuri kwa ajili ya mchezo wetu wa fainali, malengo yetu ni kuanza vizuri msimu kwa kutwaa ubingwa na kuondoka na Ngao ya Jamii," alisema Mwenda.

Naye Gamondi alisema mechi hiyo itakuwa ya ushindani na itakuwa tofauti

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >